Ufunuo, Mlango Wa Nne
Sehemu Ya I

Amina. Bwana asifiwe. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .-nyewe. Nafikiri huo ndio msimamo wa watu wengi. Ni vizuri sana, dada mdogo pale, kifungu hicho cha mwisho. Hakika nilifurahia hilo. Nasi. . .tukija kwenye usiku wa Mwaka Mpya sidhani ungeweza kuimba chochote bora zaidi, kinachofaa zaidi kwa ajili ya usiku huu.

2 Inaonekana kana kwamba tunaanza mwaka vizuri; uh-huh, nje ni kuzuri na kuna theluji na kunateleza, hali ya hewa ya kawaida ya Indiana wakati huu wa mwaka. Kwa hiyo ninyi watu kutoka Georgia ninaowaona hapa, na huko Ohio. Sasa, Ndugu Dauch, wewe na Dada Dauch mnajua hiyo ni nini, kwa kuwa Ohio ni vile vile. Na. . .bali, tunaenda kwenye Nchi ambamo hakutakuwako na yoyote ya hayo. Uh-huh. Jambo ndilo hilo.

3 Huu ni usiku wa Mwaka Mpya, mkesha. Na, loo, kila mtu ana nadhiri iliyoandikwa na ahadi utakayofanya kwa ajili ya Mwaka Mpya, kisha yapata kesho kutwa zote zitakuwa zimevunjwa. Na kwa hiyo, unajua, unafungua ukurasa mpya kila mwaka, kisha unarudi nyuma kesho yake asubuhi, ukaivunja tena.

4 Bali kuna jambo moja tu ambalo—ambalo ningetaka kusema, na hilo ni kwamba kama vile Mtume Paulo alivyosema, "Nikisahau mambo hayo yaliyo nyuma, makosa yangu yote na mambo ambayo nimefanya, ninakaza mwendo niifikie mede ya wito mkuu katika Kristo." Hayo ndiyo majuto pekee niliyo nayo ni makosa yangu ya mwaka uliopita, na sehemu iliyopita ya maisha yangu, nami ninamwomba tu kwa unyenyekevu neema nipate kukaza mwendo kuifikia mede ya wito mkuu. Nina hakika huo ndio ushuhuda we—wetu sisi sote, sote tungejisikia namna hiyo.

5 Samahani kwamba ni usiku mbaya sana na—na watu hawakuja. Nami nilimpigia simu Ndugu Neville, hata sikujua kama angeweza kufika hapa au la. Halafu Ndugu Skaggs akaja, naye anatoka huko chini kabisa Kentucky ambako kuna kina cha futi tatu ama zaidi huko chini. Na kwa hiyo. . .Ama, "Karibu *hivi*," akasema, kwa hiyo alimwomba mkulima amvurute mara kadhaa na kumfikisha kilimani kwa trekta. Na kwa hiyo nikawazia, "Vema, kama ni inchi mbili tu ama tatu, hatutajali hilo, uh-huh, mradi tu iko hivyo." Bali barabara zinapitika na kila mtu anaendelea.

6 Sasa, hakika, usiku wa leo ni usiku ambapo sisi husikia kutoka kwa wahudumu mbalimbali, wale tofautitofauti

wanaokuja huku. Na labda watakuwa wakija kutoka sehemu mbalimbali usiku wa leo, hata kufikia usiku wa manane. Nafikiri wataketi na kuona kama ninii . . . Mwaka Mpya upate kwenda . . . uingie, na wa zamani uondoke. Na kwa kawaida wanakusanyika madhabahuni na kuomba na—na kutoa nadhiri zao kwa Mungu na kufanya upya nadhiri za—zao.

7 Nilimwambia Ndugu Neville . . . Nami nilimpigia simu kuona kama alikuwa anakuja. Nilisema kama hakuja, ningejaribu kuiendeleza vizuri niwezavyo. Halafu kama asingeweza kufika hapa asubuhi, mbona, ningeendelea kufanya yote niwezayo wakati ha—hakuwa hapa. Nami nilimwambia nitajaribu usiku wa leo, nikiwazia kuhusu kutoa ujumbe wa dakika kumi na tano hivi, ama kitu kama hicho. Na, tunaona mna wahudumu wengine kadhaa wameketi hapa, wakingojea.

8 Kwa hiyo nilikuwa . . . nilifikiri ningeanza na kuendelea tu na Kitabu cha Ufunuo, nishuke tu moja kwa moja, niuchukue mlango wa 4 sasa, nianze. Na endapo hatutaumaliza wakati huu, wakati huo mwingine tutaendelea. Kisha twende kwenye wa 5, na wa 6, na jinsi tu tuwezavyo. Bwana na atusaidie kuumaliza.

9 Ninataka kusema, kabla hatujaanza, ya kwamba kulikuwako . . . nilitembelewa muda mfupi uliopita kutoka—kutoka . . . Ndugu Drummond Thom na mkewe. Huyu ni mama na baba yake wameketi hapa usiku wa leo. Nao ndio kwanza warudi kutoka Afrika ambako wamekuwa na ibada kuu za kuokoa nafsi na uponyaji wa Kiungu. Maskini mama huyu alichukua ninii yake . . . ninaamini mahali pa nyanya yake, hivi majuzi, na kufanya ibada ya magereza, nao wenye dhambi wanamjia Bwana, na kadhalika. Ilikuwa ni ajabu sana jinsi Bwana anavyowatumia hao mume na mke wachanga. Wako hapa sasa Marekani kwa muda mfupi kufanya uinjilisti kidogo.

10 Kama yeyote wenu ninyi wachungaji . . . Ninataka kumwandikia Ndugu Drummond ninii . . . Drummond, mimi, naam, mimi huchanganyikiwa na jina hilo. Kwa nini asingechukua tu jina zuri la Kiingereza na kusahau hilo? Hebu tumpe tu namba fulani, mwasemaje, kwa sababu siwezi kulitamka hilo, la. Sidhani nusu yetu tunaweza. "Drummont," nafikiri, ndiyo njia sahihi ya kulitamka; na Dada Charlotte. Kama yeyote wenu angetaka kuwa nao, hakika ningetaka kuwasikia wameingia kanisani mwenu.

11 Mama huyo, huyu Dada Charlotte, yeye ni mtoto tu. Alikuwa akitoa ushuhuda kule juu muda mfupi uliopita, kwa Meda, juu ya matukio waliyokuwa nayo Afrika, nami nawaambia ulikuwa . . . Billy, ulizirudisha nyakati za kale tena; ilisikika kama ni kuzungumza Kiafrikana. Na kwa hiyo vita vinaendelea kule kama tu vinavyoendelea hapa.

12 Kama mtu yeyote angetaka kuwa na Ndugu Drummond kwa ajili ya . . . na Dada Charlotte, kwa ajili ya kampeni kanisani

mwao, kama mngetaka, mumpigie tu Ndugu Tony Zabel pale kwenye MElrose 7-3945. Kama ukitaka kuiandika, baadhi yenu wahudumu, bila shaka ninampendekeza Ndugu. . . Kwa kuwa yeye ni mhubiri mzuri, mvulana mwaminifu, ambaye kweli anahitaji kianzio, apate kuanza. Naye hana woga, mvulana mzuri, nami nampenda sana. Sasa, kumbukeni, MElrose 7-3945. Nami nitaiacha kadi hii ndogo hapa, ambapo kama mkininii . . . Hiyo ndiyo kadi yao, na endapo huwezi kuiandika namba hiyo, vema, unaweza kuja uichukue, ama wakati wowote baada ya mapumziko katikati ya ibada mbalimbali usiku wa leo. Na mwichukue namba yao na kuwapigia simu kama mngetaka kuwa nao katika baadhi ya makanisa yenu kwa ajili ya mkutano, ama mtu fulani unayejua ambaye angetaka kuwachukua, maana wanafanya tu uamsho kote Marekani.

13 Hiyo si ni ajabu? Inabidi Afrika kuwatuma wamishenari hapa Marekani! Hapa ndipo wanapohitajika, papa hapa, zaidi ya ilivyo huko.

14 Kwa hiyo ni wangapi walio na furaha na kushangilia kwamba Bwana amewalinda kupitia mwaka mwingine? Nasi hapa, tukifika mwishoni mwa safari. Basi tunaomba ya kwamba Mungu atatusamehe dhambi zetu zote na kupungukiwa kwetu.

15 Sasa, ninataka kusema jambo hili kabla sijaanza. Nawatakia, kila mmoja wenu ninyi nyote, mwaka mpya wa mafanikio na baraka na afya ninaoweza kuwatakia. Mungu awe nanyi! Na mkue kimwili, na kiroho, na kifedha, na kimali pia. Kila kitu ambacho Mungu anaweza kuwaletea, ninaomba ya kwamba atawaletea.

16 Sasa ninaukabili mwaka mpya, mimi mwenyewe, Mungu pekee ndiye anayejua ya usoni. Nayo maamuzi yetu hayana budi kufanywa mara moja. Tuna wafanya kazi wetu wote. Ndugu Jim, pale juu, anayo tayari sasa, kwa mialiko na kadhalika kutoka kimataifa, kote ulimwenguni; tuone mahali Bwana atakapotuongoza. Na bila shaka ninaomba maombi yenu enyi watu, kuomba kwa moyo wenu wote ya kwamba Mungu kamwe hataniacha niongozwe visivyo. Mimi—mimi. . . Juu ya chochote ninachotaka kuwa, ni kuwa mwaminifu na kamwe nisiongozwe visivyo. Na sasa, nimekuwa na mwaka mzuri.

17 Mara nyingi, watu huelewa vibaya. Nao wanaposema, "Ndugu Branham, wewe ni—wewe ni. . . huendi mahali kama ulivyozoea kwenda, na kama vile hawa wahudumu wengine wanavyofanya, na kuwa na ninii yote . . . " Ni—nilijifunza jambo moja, nililojifunza kutoka kwa Biblia yetu na kutoka kwa Bwana wetu, ya kwamba Yesu hakuwa mtu wa kujitangaza. Ha—hakuwa nako, hakuwa na maonyesho. Mnaona, Yeye—Yeye hakuwa mtu wa maonyesho, hata kidogo. Wala siamini wanafunzi Wake ni watu wa kujitangaza. Kamwe hawakujifanya watu wa maonyesho.

18 Hapo ndipo nafikiri tunakosa mwelekeo sana siku hizi, (Labda ni wazo langu tu.) hata, wakati inapotubidi kufanya tamasha kuu kuhusu kila kitu, mnajua ni kwa nini, nafikiri inaonekana zaidi sana kama kwamba ni maonyesho kuliko jambo takatifu.

19 Hivi mliona katika kule kuja kwa Bwana, wale hasa waliompokea? Walikuwa ni Simeoni, hakuna mtu aliyepata kusikia lolote juu yake, bali alikuwa akimtafuta Bwana. Kipofu Ana, hekaluni. Yohana Mbatizaji, huko nyikani. Na wale . . .

20 Yohana alienda nyikani akiwa na umri wa miaka tisa, hakuonekana tena mpaka alipokuwa na umri wa miaka thelathini; huko nyikani. Na watu kama hao walioamini kisiri, na wakajiweka wanyenyekevu, walikuwa wakikutazamia kuja kwa Bwana. Wala hawakuitangaza mikutano yao na kuwalazimu kuweka matangazo makubwa ("Haya ndiyo majira! Huu ndio wakati!") na—na matangazo ya televisheni na kila kitu. Hilo ni sawa kwa wale wanaotaka kulifanya hivyo, lakini, kwangu mimi, hilo halionekani kuwa kama Kristo.

21 Ninajua wakati mmoja ndugu Zake walimwambia, kasema, "Unafanya miujiza hii na kadhalika, mbona usipande kwenda huku juu—huku Yerusalemu? Nasi tunaenda kwenye sikukuu ya Pasaka, ukawaite Kayafa kuhani mkuu, na hao wote, na uwajulishe. Ulifanye mbele zao namna hiyo, wapate kuziona kazi Zako. Na sasa, unaona, mbona kujipumbaza na kundi la wavuvi, na kadhalika, huko chini mtoni, na tabaka hilo duni la watu? Nini . . . Kwa nini usipande huku uache ulimwengu ulione?" Mnaona?

22 Yesu akasema, "Wakati wenu upo sikuzote, wakati Wangu haujaja bado." Uh-huh. Mnaona?

23 Yohana alikuwa wakati mmoja . . . Yohana Mbatizaji, Ma—Maandiko yalinena kuhusu kuja kwake. Na kusema, "Wakati atakapokuja, kwamba . . . " Mbona, Isaya alisema, yapata miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa, "Kutakuwako na sauti ya mtu aliaye nyikani." Kisha kasema, "Milima yote iliruka kama wana-kondoo, majani yote yakapiga makofi, mahali palipoinuka palishushwa, nayo mabonde yakainuliwa."

24 Unabii kama huo! Unafikiri wahudumu wa siku hiyo . . . Walipouchukua Huo, hapana shaka walisema, "Jamani! Huyo nabii mkuu atakapokuja, kila mtu atamjua. Mungu atazitandaza tu kanopi za mbingu, ushoroba wa Mbinguni utashushwa, gari la moto litashuka, bendi ya malaika imsindikize duniani."

25 Alipokuja, alikuwa ni maskini mhubiri mwenye ndevu zilizosokotana aliyejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, pamoja na kipande cha ngozi kama mshipi. Labda hakuoga kamwe; kila miezi mitatu ama minne. Huko nje nyikani, akatoka, akasimama kwenye matope, yaliyomfikia magotini, akihubiri, "Tubuni, kwa kuwa Ufalme wa Mungu umekaribia!"

Hakwenda kwenye miji yoyote. Kama mtu yeyote alitaka kumsikia, walikuja Yordani kumsikia, wale waliotaka kumsikia. Alifanya nini? Alilitikisa taifa, aliutikisa ulimwengu.

26 Kuna mtikiso unaoendelea ambao watu hawajui habari zake. Wakati Yesu alipokuja, kamwe hakujiwakilisha Mwenyewe miongoni mwa watu wakubwa. Alikuja kwa walio Wake, alikuja kwa wale waliokuwa wakimtarajia. Huko ndiko kutikiswa kunakokuja. Hivyo ndivyo anavyofanya leo hii. Roho Mtakatifu huwajilia wale ambao Mungu amewaita. Kuna mtikiso mkuu miongoni mwa Wateule. Kitu kikuu, chenye nguvu kinachoendelea, bali ulimwengu haujui chochote kukihusu.

27 Wanafikiri, haya mambo yote makuu ya madoido, na matangazo ya ulimwenguni kote, na televisheni, na mijengo ya milioni ya dola, na kila kitu, kwamba hayo ndiyo mambo yaliyo makuu. Huo ni upumbavu machoni pa Mungu. Mungu haangalii mambo makubwa. Kile mwanadamu anachokiita "cha kipumbavu," Mungu hukiita "Kikuu"; na kile mwanadamu anachokiita "kikuu," Mungu hukiita "cha kipumbavu." "Ilimpendeza, kupitia upumbavu wa kuhubiri, kuwaokoa wale waliopotea."

28 Sasa, Yohana. Unafikiri wao wanasema nini? "Yule pale maskini mlokole kule nje, jamaa wa kale anayeonekana mwenye ndevu zilizosokotana, aliyetoka nyikani amejizungushia ngozi ya kondoo. Na, mbona, yeye anasimama matopeni, miguu mitupu, huko nje ukingoni mwa Yordani, akipiga makelele kule nje. Ni nani aliyewahi kusikia kitu kama hicho?"

29 Wakati Yesu alipokuja. "Masihi, aliyezaliwa huko kwenye zizi la ng'ombe, juu ya lundo la nyasi kavu, huku—huku ng'ombe wakilia? Na—na unamaanisha akiwa na mama... Mwana haramu, wakati baba yake...Mamaye alikuwa mja mzito kabla hawajafunga ndoa, mbona, alizaliwa nje ya ndoa takatifu. Ati jamaa huyo?" Loo, jamani! Mnaona? Lakini lilikuwa ni jambo Kuu, kamwe hawakulijua Hilo. Mnaona? Hawakulijua.

30 Vivyo hivyo siku hizi Injili ni "Kuu." Nayo Injili inatikisa kuliko ilivyowahi kutikisa hapo kabla, bali inawatikisa masalia. Hiyo ni kweli, ikiwafanya tayari.

31 "Alikuja kwa walio Wake, walio Wake hawakumpokea." Aliwaambia wanafunzi Wake, "Msiende katika njia ya Mataifa, bali afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa Israeli. Na, mwendapo, yeye awapokeaye ninyi ananipokea Mimi. Mnapoingia mjini, wasiwapokee, yakung'uteni mavumbi kutoka miguuni mwenu na mwende zenu. Na amin nawaambia, itakuwa afadhali kwa Sodoma na Gomora kwenye siku ya Hukumu kuliko itakavyokuwa kwa mji huo." Na kila mmoja wa miji hiyo iliyowakataa watu hao uko katika majivu leo hii. Kila mmoja uliowapokea, ungali unasimama kama mnara-pia. Hiyo

ni kweli, mnaona. Inachukua muda mrefu kujibu; bali Mungu hujibu, usijali. Nisianze juu ya hilo, kamwe sitaingia kwenye Ufunuo. Loo!

> Loo, ninataka kumwona, niuangalie uso Wake,
> Huko nikaimbe Milele juu ya neema Yake iokoayo;
> Kwenye barabara za Utukufuni nijalie niinue sauti yangu;
> Wakati matatizo yote yanapita, na hatimaye niko nyumbani, nikafurahi milele.

32 Ninapenda hilo. Hebu tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi. Mngetaka kusimama kabla ya kufanya hivyo? Na—nafikiri . . . Biblia ilisema, "Mnaposimama, mkiomba, sameheni." Ni wangapi walio na haja ungetaka tu kuifanya ijulikane kwa mkono ulioinuliwa? Kumbukeni, Mungu anaona, Yeye anajua yote kuhusu hilo.

33 Baba yetu wa Mbinguni, tunakaribia Utakatifu Wako wa Kiungu katika Jina la Bwana Yesu, Jina hilo litoshelezalo kwa yote lililotolewa hapa miongoni mwa wanadamu, ambalo hata familia za Mbingu na nchi zote zinaitwa "Yesu."

34 Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba utapokea shukrani zetu. Kwanza, jambo la kwanza, mwaka huu unaokufa . . . tunapouacha usiku wa leo katika ibada, tukiuacha huku tukitoa sifa, tukilisoma Neno Lako na tukijua maana ya BWANA ASEMA HIVI. Ni mambo mangapi ambayo tungeweza kuweka kwenye karatasi kuyatolea shukrani! Maskini kule kuponea chupuchupu, ambako tumekuwa nako mwaka huu, ambapo Shetani angeyatoa maisha yetu, bali Wewe hujamaliza nasi bado. Kwa hiyo tungali tunaendelea. Tunaamini, Bwana, ya kwamba tumezaliwa tu na kulelewa katika ulimwengu huu tupate kukuheshimu na kukutukuza Wewe.

35 Nasi tunaomba, Baba, Wewe utatusamehe kila dhambi na kila kosa ambalo tumefanya kote safarini. Jalia tuyasahau makosa yetu usiku wa leo tunapoyakiri, tukiyazika katika Bahari ya Usahaulifu, katika Jina la Bwana Yesu, tusije tukayachimbua tena; bali sasa tukaze mwendo tukielekea kwenye hii mede, kwa ajili ya yule Mtu mkamilifu, Kristo Yesu. Tujalie hilo usiku wa leo, Baba.

36 Wakati watumishi Wako wakizungumza, kila mmoja wao, naomba uwatie mafuta kwa Roho wa Uzima, pia jalia wahubiri zaidi ya hapo awali, na kuzileta jumbe kanisani usiku wa leo.

37 Nasi tulikusanyika hapa chini ya maskini paa hili, ambalo tunashukuru kwa ajili yake, Bwana. Tunashukuru kuwa na moto wenye joto wa kuketi karibu nao, kwa ajili ya paa juu ya kichwa chetu, hayo tu ndiyo yanayohitajika.

38 Kwa maana hazina zetu haziko humu ulimwenguni, ziko katika ulimwengu ujao. Mungu, tunaziweka huko juu ambako

tunaamini wezi hawawezi kuvunja na kuiba, wala nondo hawezi kuziharibu, kwa kuwa hazina zetu ni Uzima wa Milele. Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba Wewe utatujalia tuutunze huo siku zote za maisha yetu.

39 Tufanye watumishi wanaostahili. Tuondolee maovu yote, Bwana, mambo yote yaliyopita. Yaweke. . .Jalia mashina yote ya uovu na chuki yaondolewe maishani mwetu, tupate kuwa wanyenyekevu na watamu mbele Zako. Tujalie, Bwana. Jalia tuwe na mwaka mkuu kuliko yote tuliyowahi kuwa nayo, mwaka huu ujao. Tujalie. Tupe sasa, usiku wa leo, Neno Lako tunapozingojea tena jumbe Zako. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina. Mwaweza kuketi.

40 Sasa, kwa namna fulani ni vigumu kwangu kuiona ile saa pale, nami sitaki kuwafanya ndugu zangu kungojea sana, kwa hiyo nitajaribu kuharakisha upesi niwezavyo na kuimaliza sehemu hii. Na, labda, endapo hatutamaliza, basi kesho asubuhi tutajaribu labda kuendelea, Bwana akipenda. Halafu basi iwapo Ndugu Neville hatakuja huku, ama chochote kile, vema, basi nitajaribu, Bwana akipenda, kuwa hapa kuiendeleza ibada ya shule ya Jumapili.

41 Sasa, msisahau sasa:

> Omba, omba, ndiyo njia pekee
> . . .kuyafikia maeneo ya juu;
> Omba, omba, kuomba kwa imani
> Kutazishusha baraka za Mungu.

42 Hiyo ndiyo njia pekee utakayoweza kulifanya. Hebu tuuimbe pamoja. Mwaka huu Mpya sasa. Tuna wakati mwingi sana.

> Hebu tuombe, tuombe, ndiyo njia pekee
> Ya kuyafikia maeneo ya juu;
> Omba, omba, kuomba kwa imani
> Kutazishusha baraka za Mungu.

43 Kwa hiyo kama kuomba kwa imani hushusha baraka za Mungu, na tuendelee kuomba. Nina furaha sana, usiku wa leo, tuna nyuso mpya katika Ufalme wa Mungu ambazo hazikuwamo mwaka uliopita. Na mimi, ninaendelea tu kuomba ya kwamba zitaendelea kuongezeka zaidi na zaidi wakati wote. Wala nusu haijaweza kusimuliwa jinsi itakavyokuwa upande ule mwingine.

44 Sasa, tutafungua mlango wa 4 wa Ufunuo. Kuna mtu anayehitaji Biblia? Tunazo Biblia kadhaa hapa ikiwa ungetaka kutufuata. Vema, mmoja wa mabawabu na aje huku sasa, tunazo Biblia chungu nzima hapa. Mmoja wa wadhamini, mabawabu, ama yeyote yule, aje hapa mara moja. Ndugu Zabel; hebu mwingine mmoja aje, pia. Kama ukitaka kuchukua tu pande zote mbili, na tutaenda moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa. Basi mtu yeyote anayetaka Biblia, kufuatilia pamoja

nasi, mbona, zipelekeni moja kwa moja kule na kumpa mtu yeyote anayezihitaji.

Nasi tunawatakeni mfungue sasa Ufunuo, mlango wa 4.

45 Na, sasa, kama umeketi nyuma na ungetaka kusogea hapa mbele, tuna nafasi tele usiku wa leo mpate kusogea huku. Na mjistareheshe, kisha mwingie tu moja kwa moja kwenye somo na kunisaidia kulisoma, na kulichunguza tunapokusanyika. Kuna viti huku. Ninaona mume na mke wakija. Na hivi hapa viti viwili papa hapa. Hiki hapa kimoja kwa ajili ya yule mmoja mumu humu ndani. Na papa hapa nyuma, kunavyo tu viti huku. Nadhani blowa kidogo zinafanana kila mahali.

46 Na sasa, ni wangapi waliofurahia somo letu ambalo ndio kwanza tuwe nalo, lile somo la siku nane juu ya *Nyakati Saba Za Kanisa*? Asanteni. Linanifanya kujisikia vizuri, maana kweli nilipata baraka kuu kotoka kwalo mimi mwenyewe.

47 Sasa, usiku wa leo pamoja na mlango wa 4, tunaondoka sasa, Yohana alikuwa ameunenea Wakati wa Kanisa la Laodikia. Na, katika Wakati huu wa Kanisa la Laodikia, ulikuwa ndio wakati wa kanisa uliochafuliwa kuliko zote.

48 Nasi tuliona jambo la kuhuzunisha sana katika sehemu ya mwisho ya Wakati Wa Kanisa la Laodikia, Yesu akisimama nje ya kanisa Lake Mwenyewe ambapo alikuwa ametolewa nje, akibisha mlangoni, akijaribu kurudi ndani. Si ni dhambi hiyo? Nafikiri hilo ni moja la Maandiko ya kuhuzunisha sana niliyowahi kusoma. Yesu, nje ya mlango Wake Mwenyewe, nalo kanisa Lake lilikuwa limemfukuza, Naye alikuwa akijaribu kurudi ndani kuwaokoa tu. "Mtu yeyote atakayefungua, aniruhusu kurudi nyumbani Mwangu Mwenyewe, nitakula pamoja naye naye pamoja Nami." Hilo si ni. . . hilo si ni la kuhuzunisha? Mungu wa Mbinguni, ameondolewa kanisani Mwake Mwenyewe, kwa kanuni zao za imani na madhehebu na jinsi walivyokuwa wakifanya. Kuwatoa nje. . . kumtoa nje ya kanisa, wakazikubali kanuni zao za imani.

49 Ni jambo lile lile kama lilivyokuwa wakati Yesu aliposulubiwa. Na hiyo ilikuwa ni wakati walipomkubali Baraba, mwuaji, na kumsulubisha Yesu. Wakamwachilia mwuaji miongoni mwao, ambaye alithibitishwa "mwuaji," na kumkubali. . . nao wakamkataa Yesu Kristo, Yule wa pekee ambaye angeweza kuwapa Uzima.

50 Na hilo ndilo jambo lile lile kila dhehebu, na dhehebu la Kipentekoste, linalo leo hii. Wanaona kwamba madhehebu hayo yanakufa tu mara yanapounda madhehebu. Hapajakuwapo na moja (katika—katika kurasa za historia) ambalo liliwahi kuunda dhehebu na ambalo lilipata kufanya lolote ila kufa mara moja. Ishara zote, maajabu, na karama ziliwaacha, na kila kitu kingine, mara walipounda dhehebu. Na badala ya kumkubali Bwana Yesu awape Uzima, walirudi moja kwa moja

na kumfungulia Baraba miongoni mwao tena. Hilo si ni jambo baya sana? Si ajabu Mungu aliondolewa moja kwa moja kanisani Mwake, naye amesimama, akibisha, wakati wa mwisho wa kanisa, akijaribu kurudi ndani.

51 Sasa, tunaona ya kwamba Ufunuo umegawanywa katika sehemu tatu. Ya kwanza ni milango mitatu ya kwanza, inahusu Kanisa, Ujumbe, malaika . . . kwa wale malaika wa Kanisa. Na kutoka . . . Ndipo linatoweka pale pale kwenye mlango wa 3, halionekani tena mpaka mlango wa 19, katika mlango wa 19 linarudi. Kati ya wakati huu, Mungu anashughulika na Wayahudi. Halafu, tangu wakati huo na kuendelea, ni kati ya kule kuja kwa ule mji mkuu wa Yerusalemu, na kule—kule kutiwa muhuri kwa watu wa Israeli, na kadhalika, wakati wa mwisho.

52 Sasa, basi usiku wa leo tunaondoka . . . Mara baada ya haya, Yohana alikuwa ameona . . . Katika kisiwa cha Patimo . . . Ni wangapi wanaokumbuka Patimo ilikuwa umbali gani kutoka kwenye . . . kutoka pwani? Ilikuwa ni umbali gani? Yapata maili thelathini, hiyo ni kweli, kutoka pwani. Na kuzunguka Patimo ilikuwa ni umbali gani? Mnakumbuka baadhi ya ile jiografia? Yapata maili kumi na tano kukizunguka. Na kilitumiwa na Warumi kwa kuhamishia, kuwaweka wafungwa huko nje. Naye Yohana alikuwa huko nje kwa sababu gani? Alifanya nini? Je, a—aliiba kitu fulani? La. Alikuwa . . . Je, walimweka huko nje kwa maana alikuwa akiwasumbua watu na . . . ama kufanya uovu? La. Alikuwa huko nje kwa sababu gani? Kwa ajili ya Neno la Mungu na ushuhuda wake, kwa ajili ya kuihubiri Injili.

53 Na je, lolote linaweza kumpata Mkristo pasipo kuwa ni kwa ajili ya manufaa kabisa? La, la, la. Basi kwa nini Mungu akampeleka huko nje peke yake kisiwani? Kutupatia Kitabu hiki cha Ufunuo. Mnaona, Mungu anaweza tu kuyafumba macho ya Ibilisi wakati wowote anaotaka. Sivyo? Anaweza tu kwa urahisi. Ninampenda tu. Kwa sababu, hainibidi kuwa mwerevu, mnaona. Sasa, kama ningalikuwa mwerevu, ningejaribu kusahau yote kulihusu maana ninajua hakuna mtu angaliweza kuwa mwerevu kama Yeye. Na kwa hiyo ni—ninaninii tu . . . Chochote nilicho nacho, ninajitolea Kwake na kufanya tu kile Yeye anachosema nifanye. Hivyo tu. Wakati mwingine ni kinyume sana na vile ninavyowazia ilivyo. Lakini ninajua, kama Yeye anaongoza, Yeye ni mwerevu. Anajua analofanya, sijui mimi. Kwa hiyo ninamwacha tu Yeye alifanye, mnaona, ndipo ni ninii tu . . . ni sawa. Mnaona? Kwa hiyo ninamwacha tu alifanye. Jambo ndilo hilo, Ndugu Neville. Naam, bwana, namwacha tu alifanye. Mnaona? Yeye ndiye anayejua analofanya, sijui mimi. Mnaona? Kwa hiyo sijaribu kuwa na mapambo makubwa sana na kadhalika. Na kujinyenyekeza tu, na kusema, "Mimi hapa, Baba, wakati wowote unaponitaka." Kwa hiyo ninaendelea moja kwa moja namna hiyo na siku zote linatokea vizuri.

54 Kwa hiyo, Yohana, tusingekuwa na Ki—Kitabu cha Ufunuo kama haikuwa ni Yohana, na kama Yohana asingalikwenda huko kisiwani. Hiyo ilikuwa ni njia ya Mungu ya kutupatia Kitabu cha Ufunuo. Alikuwa huko nje, nafikiri, yapata miaka mitatu, na juu ya kile Kitabu . . . akaandika Kitabu cha Ufunuo.

55 Sasa, ndipo tunapomwacha kwenye ule mwaliko wa mwisho, wa kifungu cha 22 cha mlango wa 3, "Aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."

56 Sasa, tuanzie mlango wa 4:

> *Baada ya hayo, naliona, na tazama, mlango ukafunguliwa mbinguni: na sauti ile ya kwanza niliyoisikia kama . . . sauti ya baragumu ikinena nami, ikisema, Panda hata huku, nami nitakuonyesha mambo ambayo hayana budi kuwako baada ya hayo.*

57 Tutalichukua kifungu baada ya kifungu. Nami nina Maandiko mengi sana yaliyoandikwa hapa chini, kitabu kizima, na sijui tutafikia umbali gani Kwake. Bwana na atuongoze. Sasa, angalieni, Neno ni:

> *Baada* ya haya (baada ya wakati wa Kanisa) . . .

58 Na haya yote tangu sasa, sasa, yatakuwa yanahusu, yatatukia duniani baada ya ule Unyakuo wa Kanisa. Mnaona, baada ya ule Unyakuo. Hii inarudi tena sasa kuwachukua Israeli. Baada ya wakati wa Kanisa, baada ya nyakati za Kanisa, nazo . . . Kanisa halionekani tena mpaka Ufunuo mlango wa 19 wakati linaporudi pamoja na Bwana-arusi Wake. Mungu asifiwe kwa ajili ya Arusi!

59 Hebu tusome tu hilo. Mngetaka kuyasoma Maandiko haya wakati tukiendelea? Vema. Hebu tufungue Ufunuo 19. Vema, bwana, Ufunuo 19. Hebu tuanzie kwenye kifungu cha 7, Ufunuo 19. Huu ni wakati Kanisa litakapoonekana tena, halionekani tena mpaka kwenye mlango wa 19.

> *Na tufurahi tukashangilie, tukampe utukufu wake: kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari.*

60 Loo, ni—ningeweza kuhubiri juu ya hilo hadi usiku wa manane na hata nisiyasimulie nusu. Angalieni, "Mkewe amejiweka tayari."

61 Charlie, Nellie, nanyi nyote, ni yale tu tuliyokuwa tukizungumzia, huko chini, na Rodney, hivi majuzi. Mnaona? Wakati Elisha alipolitupa vazi hilo juu ya Eliya . . . Ama Eliya alipolitupa juu ya Elisha; alinyosha mkono akalichukua tena, akalivaa na kutembea nalo hata akavuka Yordani, kisha akapanda mlima na kupanda gari la farasi, akalishusha tena.

62 Mkristo anapookolewa mara ya kwanza, uso wake unaelekezwa kwa Kristo, ndipo ana jambo la kufanya yeye mwenyewe. Inambidi, jambo la pili, kujitakasa na tabia zote

chafu, “akiweka kando kila mzigo mzito, akijiweka Mwenyewe tayari. Bibi-arusi amejiweka tayari Mwenyewe!”

63 Inanikumbusha juu ya hadithi ndogo, sina budi tu kuisimulia kabla hatujaendelea. Huko Magharibi huku, wakati fulani uliopita, miaka mingi, kulikuwako na Armour and Swift Packing Company iliyokuwa mashuhuri. Jinsi wanavyofanya, wanakuja huko nje na kununua ng’ombe na kununua maranchi. Nao ni matajiri sana, nao wananunua ranchi zote ndogondogo, na wana mamilioni ya ekari za ranchi namna hiyo, wanawafuga hawa ng’ombe wakubwa wazuri wa Herefodi, sehemu sehemu. Ninii yao. . . Wanamiliki reli zao na kadhalika zinazowaleta hao ng’ombe kutoka malisho moja hadi mengine.

64 Basi Armour and Swift walikuwa na ranchi kubwa, na siku moja walikuwa na msimamizi pale, mwangalizi, alikuwa, wa hiyo ranchi, alikuwa na yapata binti wanne ama watano. Basi wakagundua ya kwamba mmoja wa ndugu wakubwa wa Armour alikuwa. . . ama, sio ndugu, bali wana, walikuwa waitembelee hiyo ranchi. Naye alikuwa ki—kijana, mseja. Nao wasichana hawa wote walikuwa na hakika watamvutia mvulana huyu mara tu a—akija. Nao kwa hiyo wote walikuwa wakijiandaa na kufanya kila kitu tayari kuja.

65 Alipofika kule, walikuwa wamlaki na kufanya sherehe za kale za mipakani, huku wamevaa maskini nguo zao ndogo, zenye matamvua, na za .44 kwenye kila nyonga, na hizo kofia nyuma ya kichwa chao, mwajua. Nao walikuwa wajifanye wa kimagharibi wa kawaida, na kila mmoja wa hao wasichana angepata. . . Mmoja wao angempata mvulana huyu.

66 Basi walikuwa na ma—maskini binamu yao mdogo pale ambaye mama yake alikuwa amekufa na baba yake amekufa. Alikuwa ni binamu, na karibu alikuwa ndiye mtumwa wa wote waliokuwa kule. Na kazi yote chafu, ilimbidi kuifanya, kuosha vyombo na kila kitu. Naye hakuwa na nguo, ilimbidi kutegemea za kuachiwa na. . .

67 Kwa hiyo wakati ulipowadia wa huyo mvulana kuwasili, wote walikuwa na mikokoteni yao ya farasi na, wakaondoka, moja kwa moja kwenda stesheni kumlaki. Nao walikuwa wakirusha risasi, huku farasi wakilia na kadhalika. Basi wakamleta kwenye ranchi. Na usiku huo walikuwa na sherehe kubwa. Ndipo wakaenda huko nje kwenye malundo ya nyasi kavu na uzio wa boma, na wao—wao wakaimba na kucheza dansi, na kote usiku kucha. Alikuwa kule kwa siku mbili ama tatu.

68 Maskini binamu huyu. . . Sasa, nitafananisha hili na kitu fulani sasa. Binamu zetu ambao wamevalia kwelikweli, minarapia mikubwa na makanisa mazuri, na inaonekana kana kwamba endapo kuna jina lolote chafu halina budi kupewa wapentekoste, kitu kibaya. Wao hufanya kosa pia, bali hakuna lolote

linalosikika, mnaona. Wao kwa namna fulani ni wangwana, kwa hiyo wao. . .husikii kuhusu hilo. Lakini acha mhudumu fulani wa Kipentekoste afanye kosa wakati mmoja, na, ndugu, nakwambia, watalieneza kote nchini katika kila gazeti. Naam, bwana. Acha ndugu fulani wa kipentekoste amwombee mtoto, naye afe, kila gazeti nchini litalitangaza, "Uponyaji Wa Kiungu Ni Ulokole."

69 Vema, basi mbona wasiweke kila kisa gazetini ambacho daktari anapoteza? "Sheria ni msumeno, yakata mbele na nyuma." Mnaona? Kwa hiyo, kama wangefanya hivyo, wasingekuwa na nafasi ya kutosha kwenye magazeti kuwaorodhesha wafu wote. Kama ningetoka niende hapa nje makaburini na kusema, "Kila mtu aliyepata kufa chini ya uponyaji wa Kiungu na asimame," kisha niseme, "Kila mtu aliyepata kufa chini ya matibabu ya dawa na asimame," wangewashinda idadi milioni moja kwa mmoja. Na hiyo ni kweli kabisa. Kwa hiyo kama watamkosoa mmoja, wamkosoe mwingine. Kwa hiyo hiyo ni kweli. Bali wao wanawaua mamilioni kwa mwaka kwa dawa na upasuaji, wala husikii neno juu yake. Mnaona?

70 Kwa hiyo, maskini msichana huyu mdogo, alikuwa na kazi zote ngumu kufanya. Kwa hiyo wakati, mara moja, yule mvulana. . .usiku mmoja baada ya chakula cha jioni kwisha na walikuwa wamecheza dansi, na kila mmoja wa wasichana hawa alikuwa amejirembesha vilivyo, mwajua. Basi maskini msichana huyu ilimbidi kuvaa maskini nguo mbovu, ya kale, iliyochakaa. Ndipo usiku mmoja alikuwa ameketi kwenye ukumbi wa chakula baada ya chakula cha jioni kwisha, naye alikuwa ameviosha vyombo na alikuwa amekimbia nyuma ya ua kumwaga maji ya kuoshea vyombo. Yeye. . .alipogeuka kwenye ule uzio wa boma, huyo hapo amesimama, ameegemea kwenye uzio wa boma. Akasema, "Aloo."

71 Aliaibika sana, kwa sababu huyo alikuwa ni mwana wa msimamizi, mwana wa mwenye ranchi. Akaiinamisha sufuria ya vyombo, asije akamwona amevaa matambara; akaanza kurudi nyuma, miguu mitupu, akiangalia nyuma, namna *hii*.

72 Basi akamwendea, kasema, "Usiniogope." Kasema, "Ninataka kukwambia jambo fulani." Akasema, "Nilikuja huku kwa kusudi moja, nimekuja kutafuta mke." Kisha kasema, "Nimekuwa nikitafuta kila mahali." Kasema, "Sikutaka kuoa yeyote wa hao wasichana huko mjini, ninataka kupata niliyefikiri ni mke halisi." Kisha kasema, "Katika wote ambao nimewaona, nimekuwa nikikuona wewe mahali hapa. Nami nimepata kujua kupitia watu wengine kwamba wewe ni binamu."

Kasema, "Hiyo ni kweli, bwana."

73 Kasema, “Nataka kukuuliza jambo fulani. Je, utakubali nikuoe?” Mbona, hakujua la kufanya. Alikuwa amechanganyikiwa sana, hakujua—hakujua jinsi ya kumjibu mtu huyo.

74 Loo, karibu tu niwazie alivyojisikia. Nanyi je? Wakati mimi, wakati mmoja nikiwa mwenye dhambi, sifai kitu, mtoto wa mlevi, Yesu Kristo akasema, “Ninakutaka uwe Wangu.” Angewezaje kamwe kumjia mtu kama mimi? Angewezaje kusema kamwe, “Nitakupa makao Mbinguni”? Angewezaje kusema, “Nitakuokoa”? Mwovu kama mimi, ingewezekanaje? Lakini alilifanya!

75 Akasema, “Bwana, si—mimi si—si—sistahili. Nisingeweza kuwa mke wa mtu kama wewe,” kasema, “kwa sababu umezoea mambo makubwa. Wala mimi sijui kitu kuyahusu, mimi ni maskini.”

Akasema, “Lakini wewe ndiwe chaguo langu.”

76 Basi si lilikuwa ni jambo zuri wakati Yesu alipokwambia hivyo . . .? Ulijua hukustahili kuwa Mkristo. Wewe, hapakuwapo na jambo ungaliweza kufanya, bali Yeye . . . Si kitu . . . Yeye—Yeye alikuchagua tu. Mnaona? Yeye . . . Ni wema Wake, rehema Yake ambapo alikuchagua. Hukumchagua Yeye, unajua, Yeye alikuchagua. Hiyo ni kweli.

Akasema, “Si—sininii . . . ” Akasema . . .

77 “Usiziangalie nguo zako. Mimi siziangalii nguo zako, ninaangalia kile ulicho.” Akasema, “Je, utakubali nikuoe?” Na hatimaye mapatano yakafanywa. Naye akasema, “Mwaka mmoja tangu leo, nitarudi. Uwe tayari. Uvae vazi la arusi, kwa kuwa nitarudi na kukuoa papa hapa mahali hapa. Nami nitakupeleka Chicago, huko Outer Drive, huko ambako utakuwa na kasri la kuishi. Na huku kuosha vyombo kwote kutaisha, na kadhalika, wakati huo.”

78 Wakati wale dada, ama binamu, waliposikia hivyo, walisema, “Wewe maskini, mjinga, mdogo! Mbona, unajua mtu huyo hakumaanisha hilo!”

79 Basi si hivyo ndivyo hasa wanavyosema leo hii? “Lingewezaje kundi la watakatifu wanaojibingirisha, kundi la watu ambao ni vigumu kwao kuandika jina lao, wangewezaje kamwe kuwa ndio Kanisa? Kundi kama hilo kamwe lingewezaje kuwa?” Lakini hilo ni sawa tu. Wakati tulipoposwa na kuhisi hilo busu la posa la Yesu Kristo moyoni mwetu kutuondolea dhambi yetu, kitu Fulani kinatwambia ya kwamba Yeye anarudi tena, hakika kabisa. Siku moja atarudi.

80 Mwaka mzima alifanya kazi, kwa nguvu sana, akiweka akiba hapa maskini senti zake sabini na tano, kile—kile wanacholipa hapa kama ujira wake kwa siku. Naye alikuwa akiweka akiba fedha zake apate kununua vazi lake la arusi, kuandaa kila kitu.

Loo, hayo ndiyo yaliyokuwa mawazo yake yote, kujifanya tayari. (Naye ameninii . . . "Amejiweka tayari Mwenyewe.") Akapata nguo zake, nguo zake za arusi, wakati binamu zake wakimcheka na kumdhihaki.

81 Hatimaye ikafikia . . . hatimaye ile siku. Akavaa vazi lake la arusi (Loo!), akajitayarisha na kuoga. Nao maskini binamu zake wakaja pale na kuinama karibu naye na kusema, "Vema, maskini mpumbavu wee. Mbona, unajua yeye hakumaanisha hilo. Asingezungumza na . . . asingeoa msichana kama wewe." Bali, alijiweka tayari, kwa vyovyote vile.

82 Kwa hiyo ikafika jioni kabisa, nao wakaanza kumdhihaki na kumtania. Akasimama papo hapo mlangoni, akingojea, kwa vyovyote vile. Na kwa hiyo yeye . . . akasema, "Kwani alisema atakuwa hapa saa ngapi?"

83 Kasema, "Hakusema." Lakini kasema, "Aliniambia . . . aliniambia ule usiku ambao atanioa . . . ama alinipa pete ya posa. Yeye alisema, aliniambia, 'Itakuwa yapata mwaka mmoja tangu sasa.' Kwa hiyo ninayo saa moja iliyosalia." Amina, akaendelea tu kungojea, "Nina saa moja iliyosalia, dakika thelathini zilizosalia, dakika kumi zilizosalia." Nao wakamcheka na kumdhihaki, na kumwita kila kitu.

84 Lakini, hatimaye, papo hapo kwenye hiyo saa iliyo muhimu sana, wakasikia changarawe zikibingirika chini ya magurudumu, farasi wakija. Lilikuwa ni jambo la jinsi gani kuona maskini bibi-arusi huyo aliyejiweka tayari, akiruka kutoka mlangoni, na kukimbia kupitia kwenye vijiti vilivyofunikwa na waridi huko nje, kuruka mikononi mwa mtu aliyempenda, na atakayekuwa mume wake, amchukue namna hiyo, akaolewe kisha waende zao.

85 Baadhi ya siku hizi, ndugu, wale wanaodhihaki na kusema "mtakatifu anayejibingirisha," na—na "mpentekoste," na mambo kama hayo . . . Tunangoja, tungali tuna muda kidogo. Wao wanasema, "Ah, hakuna tofauti na vile ilivyowahi kuwa." Usijali, tuna muda mfupi uliosalia. Na kwenye wakati ule ambao aliahidi, Yeye atakuwa hapa. Na baadhi ya siku hizi tutaruka na kuondoka. Iweni tu tayari! Vaeni Vazi la Arusi! Ondoa ukatili wote moyoni mwako. Kila kitu ambacho . . .

86 Sikiliza jinsi Andiko hili linavyosema hapa:

> *Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake: kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari.* (Mnalipata?)
>
> *Naye amepewa kuvikwa kitani nzuri, ing'arayo, safi: kwa maana kitani nzuri ni matendo ya haki ya watakatifu.* (Mungu asifiwe!)

Naye akaniambia, Andika, Heri walioalikwa karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo. Akaniambia, Maneno haya ni maneno ya kweli ya Mungu.

87 Kwa hiyo kutakuwa na mkutano hewani moja ya siku hizi, kwenye kipindi kitamu, kitamu hivi karibuni. Uh-huh. Iweni tu tayari! Jiwekeni tayari! Utakase moyo wako kutokana na mawazo yote maovu. Mwamini Mungu, haidhuru kunaonekana giza jinsi gani na kuna vicheko vingapi na dhihaka ngapi na kusema, "Umekosea." Endelea tu kuishi mtakatifu na kumwishia Mungu. Endelea tu kusonga mbele, ile saa itafika!

88 Kwa hiyo, mnaona, anatokea tena sasa katika Ufunuo 19:

Baada ya hayo...(Akiisha kuuona wakati wa Kanisa.)

Baada ya mambo haya *naliona, na, tazama, mlango*...

89 Sasa, kumbukeni, Yohana angali kwenye Patimo. Na baada ya kuziona nyakati zote za kanisa zikipita:

...naliona, na, tazama, mlango ukafunguliwa mbinguni:...

90 "Mlango." Mlango ni kitu gani? Ufunuo 3:8. Katika Ufunuo, mlango wa 3 na kifungu cha 8, "Najua matendo yako. Tazama, nimeweka mbele zako Mlango uliofunguliwa ambao hapana mtu awezaye kuufunga, naweza kuufunga na hapana mtu awezaye kuufungua." Yeye ndiye Mlango! Mlango! Kristo ndiye Mlango. Yeye alisema, katika Yohana Mtakatifu 10, "Mimi ndimi Mlango wa zizi la kondoo."

91 Na katika nchi ya kale, unakuta kwamba mchungaji huwaingiza kondoo wake. Akiisha kuwahesabu na kuhakikisha kwamba wote wako ndani, ndipo anajilaza papo hapo mlangoni. Mbwa mwitu hawezi kuingia pasipo kumwamsha, wala kondoo wake hawawezi kutoka nje pasipo kumkanyaga. Loo, jinsi kondoo wanavyojisikia salama kwa kuwa mchungaji amelala mlangoni.

92 Nuhu, katika Agano la Kale, alisimama katika mlango wa safina. Loo, sikilizeni; nitasema jambo fulani! Alisimama mlangoni akawahubiria toba na haki watu waliomcheka. Na kwenye mlango uo huo aliposimama, hakuna mtu angaliweza kuingia kwenye safina ila kwa mlango huo mmoja. Hapakuwapo ila na mlango mmoja kwenye safina.

93 Na kuna Njia moja tu! Vema, Ndugu...?...Kuna Njia moja tu iingiayo katika Mwili wa Kristo. Kuna Mlango mmoja tu wa kuingia katika Kanisa la Mungu aliye hai, na Yesu ndiye huo Mlango! "Mimi ndimi Mlango! Mimi ndimi Njia, ile barabara inayoelekeza kwenye Mlango. Mimi ndimi Mlango wa zizi la kondoo."

94 Yeye aliuambia wakati huu wa kanisa, "Nimeweka mbele yako Mlango uliofunguliwa." Alisema hayo kwa wakati wa kanisa la Methodisti, wakauacha, wakaingia katika dhehebu. "Lakini nimeweka mbele zako Mlango uliofunguliwa." Sasa, wakiisha kupokea utakaso, Yeye alisema, "Nitaweka Mlango uliofunguliwa," ambao ni Roho Mtakatifu. "Kwa Roho mmoja sisi sote" (vipi?) "tumebatizwa kuwa Mwili mmoja ambao ni Kristo." Yeye aliuweka ujumbe huo mbele ya kanisa la Methodisti nao wakauacha. Walifikia utakaso kisha wakamkataa Roho Mtakatifu. Mnakumbuka hilo? Huo "Mlango uliofunguliwa."

95 Unaingiaje ndani ya Kristo? Kwa Roho mmoja, Roho Mtakatifu, ambaye ni Roho wa Kristo. Tumeingia, si kwa kupeana mkono, sio kwa kunyunyizia, bali kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu mmoja tumebatizwa sote kuwa Mwili mmoja na kufanywa washiriki wa Mwili huo. Ubatizo wa Roho Mtakatifu mmoja kuingia katika huo Mlango.

96 Mlango huu umewekwa Mbinguni, Mlango huo, wakati alipoangalia juu alimwona Bwana Yesu. Angalieni tu hii sehemu yake nyingine. Mlango huo, Bwana Yesu.

> . . .*naliangalia, na, tazama, mlango ukafunguliwa mbinguni, na sauti ile ya kwanza*. . .*niliyoisikia ilikuwa*. . .sauti *ya baragumu*. . .

97 Sasa mandhari inabadilika. Yohana amekuwa akiangalia Patimo, na sasa anaangalia juu. Kwa nini? Ameona kitu kilichoendelea hapa duniani (hizi nyakati za kanisa), kote katika Nyakati Saba za Kanisa, kisha baada ya kumaliza kuona nyakati hizo za kanisa, baadaye, baada ya kumalizika kwa nyakati za kanisa, alisikia Sauti. Ndipo akaangalia juu Mbinguni akaona Mlango uliofunguliwa, nayo Sauti ya kwanza ilisikika kama baragumu. Vema, mandhari ikabadilika kutoka Patimo ikawa Mbinguni.

98 Sauti ilikuwa ni Sauti ile ile iliyotembea katikati ya vile vinara vya taa saba vya dhahabu; Sauti ile ile, hiyo Sauti haikubadilika. Lakini, ile Sauti, ilikuwa wapi wakati alipoisikia kwa mara ya kwanza? Ni wangapi wanaokumbuka, katika wakati wa kwanza wa kanisa? Nyuma yake. "Nilikuwa katika Roho siku ya Bwana," Ufunuo 1—1:10. Kwa hiyo yeye . . . "Katika Roho." Ukitaka kuandika hilo katika Ufunuo 1:10 na 13, "Nilikuwa katika Roho siku ya Bwana, nikasikia nyuma yangu Sauti kama ya baragumu nayo ilisikika kama maji mengi. Ndipo nilipogeuka kuangalia, nilimwona Mmoja amesimama katikati ya vinara vya taa saba vya dhahabu."

99 Sasa, akiisha kumwonyesha siri hiyo yote ya hivyo vinara vya taa saba vya dhahabu (ameshika zile nyota saba, na amevaa wigi nyeupe, na kadhalika, na miguu kama shaba, na macho kama moto, hiyo mifano), ndipo aliposikia Sauti

ile ile (Angalieni.) ikinena kutoka Mbinguni. Basi akaangalia juu akaona Mlango uliofunguliwa. Loo! Mlango uliofunguliwa Mbinguni! Unaingiaje mle? Kwa Kristo Yesu, Mlango huo mmoja, Njia moja, hakuna njia nyingine.

100 "Mtu yeyote anayeingia kwa njia nyingine yoyote, huyo ni mwizi na mnyang'anyi." Na kwenye ule mfano wa yule aliyepanda juu naye alikuwa kwenye Karamu ya Arusi bila ya kuvaa vazi, alipatikana na hatia, ndipo akafungwa na kutupwa katika giza la nje. Njia moja pekee, ya kuja kwenye Karamu ya Arusi. Ninaamini nilihubiri juu ya hilo hapa si muda mrefu uliopita. Wakati wowote bwana-arusi . . . Wakati mtu alipopata . . . anapooa kwenye nchi ya kale, hana budi kutoa mialiko mwenyewe, inambidi kutoa mavazi rasmi mwenyewe. Kwa hiyo alipokutana na mtu huyu pale, yeye ameketi kwenye meza ya chakula cha jioni . . . Ni wangapi wanaokumbuka mfano huo? Hakika, ninyi mnaoisoma Biblia. Basi akampata mtu kwenye meza ya chakula cha jioni asiye na vazi la arusi.

101 Ni kitu gani? Bwana-arusi husimama mlangoni na wote wanakuja na mwaliko. "Hakuna mtu awezaye kuja Kwa Baba isipokuwa kwa njia ya Mimi. Wote alionipa Baba, ama walioalikwa, watakuja Kwangu." Hawa hapa wanakuja, wanatoa mwaliko wao, bwana arusi, kusudi kila mtu afanane na mwingine. Hilo ndilo jambo moja kuhusu ile dini nzuri ya mtindo wa kale ya Roho Mtakatifu, inawafanya wote wafanane. Kama ni matajiri ama maskini, wafungwa ama walio huru, weusi ama weupe, wanaume ama wanawake, wote ni mmoja katika Kristo Yesu. Basi bwana arusi alisimama mlangoni na kupokea mwaliko, akamvisha jamaa huyu vazi rasmi, kwa hiyo matajiri na maskini wote walifanana. Hivyo ndivyo ilivyo katika Ufalme wa Mungu, hakuna jamaa wakubwa wala jamaa wadogo; wote ni jamaa mmoja, wote ni mmoja katika Kristo.

102 Sasa, unaonaje wakati Bwana-arusi aliporudi na kumwona mtu ameketi pale bila Vazi la Arusi? Kasema, "Rafiki, uliingiaje humu?" Ndipo akasimama ameduwaa, ilionyesha ya kwamba alipitia njia nyingine mbali na ule Mlango. Alipitia dirishani, alipitia mlango wa nyuma. Naye alimwita rafiki, ilionyesha alikuwa ni mfuasi wa kanisa, "Rafiki, uliingiaje humu bila vazi?" Sasa, Yesu alisema hivi, Yeye Mwenyewe. Ndipo akamwita bawabu, akasema, "Mfunge, mguu na mkono." Naye akatupwa kwenye giza la nje ambako kutakuwa na kulia, kuomboleza, na kusaga meno. Hayo ni Maneno ya Kristo Mwenyewe, (Kweli.) "Alitupwa nje." Kwa sababu, ilithibitika, pasipo na Vazi la Arusi, yeye alipitia njia nyingine mbali na ule Mlango. Kama angalipita kwenye Mlango, angalipokea Vazi la Arusi.

103 Loo, sikilizeni hili! Basi ikiwa Vazi la Arusi ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, tutawakilishwaje kwa njia nyingine yoyote? Ikiwa wakati wa kwanza wa kanisa ilibidi uje kupitia Mlango huo, Kristo Yesu, kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo,

kuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuvaa Vazi la Arusi, tunakujaje kwa njia nyingine yoyote? Ukija kwa njia ya Methodisti, kwa ya Baptisti, ama kwa ya Wapentekoste, ama dhehebu lingine lolote, utafungwa na kutupwa kwenye giza la nje. Huna budi kuja kwa njia ya Kristo Yesu, Njia, Mlango, Kweli, Uzima. Amina!

104 Vema, Sauti ile ile, Ufunuo 21, ama, Ufunuo 1:10 na 13. Nami ninawatakeni muone, ile Sauti aliyosikia ikizungumza naye ilikuwa na udhahiri wa baragumu. Mnajua jinsi baragumu inavyolia, inatoa sauti kali. Baragumu inamaanisha nini katika Biblia? Vita. Wakati wowote unapoona baragumu ikipigwa, katika vita . . . katika wakati wa Biblia, sauti yake ilimaanisha vita, ama ufunuo fulani ama jambo fulani litakalotukia.

105 Sasa, yeye . . . Baada ya zile nyakati za kanisa kumalizika, na kila kitu kuwekwa tayari, iliweka tayari yale mandhari ya mlango wa 4 hapa, nyakati za kanisa zilikuwa zimekwisha. Alikuwa tayari ameondoka duniani, mnaona. Kumbukeni, ile Sauti iliyonena naye, nyuma yake, kwenye vile vinara vya taa saba vya dhahabu, kazi ilikuwa imemalizika. Na sasa Sauti ile ile ilikuwa ikinena huko juu Mbinguni. Ilikuwa ni nini? Alikuwa tayari amewakomboa watu Wake. Kazi Yake ya duniani ilikuwa imekwisha, Naye alikuwa Utukufuni, akimwita Yohana, "Njoo huku juu!" Uh-hum. Amina! Hilo linanifanya nijisikie kupiga makelele kwenye mkesha wa Mwaka Mpya. Loo, jamani! Haya basi. Mnaona, tayari, "Njoo huku juu!"

106 Vita! Haya ndiyo mandhari ya vile vita vikuu; watu walioukataa Ujumbe wa Mungu, waliomkataa Roho Mtakatifu, yule Mjumbe wa yale makanisa saba. Wale waliokuwa wameukataa Ujumbe huu wa neema Yake hawakuwa na kitu kilichosalia, lakini hukumu ilikuwa tayari; loo, wakati alipokuwa akijiandaa kumwaga yale mapigo juu ya nchi sasa. "Njoo huku juu na Mimi nitakuonyesha yale yanayokaribia kutukia. Wenye dhambi wanaomkataa Kristo, wasio na Mungu, nitaimwaga ghadhabu Yangu juu yao."

107 Angalieni yale mandhari yake. Loo, tunapoendelea usiku mtaendelea kupata zaidi ya hayo na zaidi ya hayo wakati wote. Hatuwezi kuingiza kila kitu hapa, inatubidi kuendelea kurejea mahali mahali. Jinsi ambavyo litakuwa ni jambo la kuchukiza mno kwa hao wakati baragumu ya mwisho itakapolia, na wakati vita vya mwisho vimepiganwa, wakati mahubiri ya mwisho yamehubiriwa, wakati wimbo wa mwisho umeimbwa, nasi tusimame kwenye Kiti cha Hukumu cha Kristo. Utaulizwa, "Kwa nini hukulipokea? Ulifanya nini na Uhai niliokupa?" Utaulizwa kutoa sababu yake. Vipi basi?

108 Mumenisikia nikiimba wimbo huo, ama kuujaribu:

Vipi basi? Vipi basi?
Wakati kile Kitabu kikubwa kitakapofunguliwa, vipi basi?
Wakati wale wanaoukataa Ujumbe
Wataulizwa kutoa sababu, vipi basi?

109 Utasimama pale, hakika tu kama vile Kitabu hiki kilivyoandikwa. Utakuwa...utasimama pale na kuulizwa sababu. Loo, inatufaa sisi, ndugu yangu, dada, inatupasa, kama wana na binti za Mungu, kujichunguza kila saa ya siku. Paulo alisema, "Mimi hufa kila siku. Hata hivyo ni hai, si mimi, bali Kristo anaishi ndani yangu." Mnaona? Jichunguze, kwa kuwa hujui ni wakati gani utakapoitwa kujibu huko Juu.

110 Sasa, "Kasikia Sauti ya baragumu." Vema. Angalia, angalia yale Yohana aliyosema, aliyosema hapa, katika sehemu ya mwisho ya mlango huu wa kwanza:

> ...*sauti ile ya kwanza*...*ilikuwa*...kama *sauti ya baragumu* ikinena *nami, ikisema, Panda hata huku*,...

Panda hata huku! Nilikuonyesha nyakati za kanisa duniani; sasa njoo huku *juu*, nitakuonyesha jambo linalotukia huku juu.

111 Mnaona, Kristo alikuwa ameondoka duniani wakati huo, alikuwa ameenda juu Utukufuni, wakati wa Kanisa ulikuwa umekwisha, ilionyesha kwamba Roho Wake alikuwa amemaliza kazi hapa. Naye alikuwa ameenda Utukufuni na alikuwa akimwita Yohana apande juu, Naye akamwonyesha yale mengine yatakayotukia. "Panda hata huku."

112 Sasa, tunaona Yohana, mlango wa pili...kifungu cha pili. Angalieni upesi, Yohana aliongezea hivi:

> *Mara*...(Amina!)

113 Loo, kama nikitenda kigeni, ninajisikia vizuri tu. Yohana aliongezea:

> ...*mara nalikuwa katika roho:*...

114 Unaposikia Sauti ya Mungu ikisema nawe, jambo fulani linatukia. Amina! Loo, lilitukia kwako namna hiyo? Lilitukia kwangu, miaka thelathini na mmoja iliyopita, na kamwe sijawa yule yule tangu wakati huo. Loo, wakati Yeye aliposema, "Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye mizigo mizito, nitawapa pumziko." Lilinibadilisha.

115 Yohana akasema:

> ...*mara nalikuwa katika roho*:...(Roho gani? Roho Mtakatifu. Loo!)...*nalikuwa katika roho: na tazama kiti cha enzi kimewekwa mbinguni na mmoja ameketi juu ya* kile *kiti*.

116 Mnaona, Yohana alikuwa ameondoka duniani sasa. Kristo alikuwa ameondoka duniani (katika umbo la Roho Mtakatifu) na alikuwa amerudi kwenye ule Mwili tena. Leo hii huo Mwili

umekaa pale kama kumbukumbu, kama dhabihu. Tutafikia hilo papa hapa chini kwenye mlango huu hapa. Lakini Roho wa Kristo alirudi apate kuishi ndani ya Kanisa, kuishi ndani yetu.

117 Sasa, mara baada ya kuonyesha mwisho wa wakati wa kazi Yake hapa, Yeye alipaa juu Mbinguni, Akasema, "Nitakuonyesha yatakayotukia baada ya haya, baada ya nyakati hizi za kanisa." Akasema, "Yohana, siwezi kuzungumza nawe huko chini tena, maana nimeondoka huku chini, nimepanda huku juu zaidi. Panda hata huku juu pamoja Nami!" Amina! "Nami nitakuonyesha yatakayotukia baada ya haya." Loo, jamani! Hmm! Loo! Akatwaliwa katika ono, akanyakuliwa hata Utukufuni.

118 Ujuzi wake hapana shaka ulikuwa kama ule wa Paulo. Wakorintho wa Pili 12:2 na 4, kama mnaliandika. Wakorintho wa Pili . . . 2 hadi 4. Paulo alinyakuliwa siku moja, katika . . . katika ono, pia. Mlijua hilo? Naye akaona mambo ambayo haikumjuzu yeye hata kuyasimulia; kwa miaka kumi na minne, hata hakuligusia. Mnaona? Bali sikilizeni tofauti kati yao.

119 Kile Paulo alichoona, alikatazwa kukizungumzia wala kukitangazia umma. Loo, jamani! Siamini angefanya hivyo. (Kwa kuwa, ziara ndogo niliyofanya siku moja, sijaweza kuisahau wala sitaisahau kamwe.) Mnaona, a—aliona mambo ambayo hangeweza kuyazungumzia. Nadhani hakuwa na maneno ya kuninii . . . alinyakuliwa mpaka mbingu ya tatu, hata hivyo. Mnaona, mpaka Mbingu ya tatu.

120 Ni tofauti jinsi gani wakati Yohana aliponyakuliwa na kumwona Yesu, alikuwa . . . Kasema, "Andika kwenye kitabu kile umeona na kukirudisha, ukayatumie makanisa." Paulo alikatazwa kunena, hali Yohana hata aliombwa kuyaandika kwenye kitabu kusudi yapitie kote kwenye nyakati. Loo, jamani! Yamefunuliwa sasa, yakafunuliwe katika siku hizi za mwisho. Hayakufunuliwa katika siku zake, yanafunuliwa sasa tunapoendelea.

121 Loo, pia angalieni, Yohana, akinyakuliwa mara baada ya wakati wa kanisa, alikuwa ni mfano wa Kanisa lililonyakuliwa. Mara baada ya wakati wa kanisa kumalizika, Wakati huu wa Kanisa la Laodikia, ndipo unakuja Unyakuo. Kanisa linapanda juu kama Yohana alivyofanya, kuingia Uweponi mwa Mungu. Loo, jamani! Whiu! Hilo linaizungusha tu nafsi yangu. Kunyakuliwa, kwenye ule Unyakuo wa Kanisa! Nalo lilisema . . . Mahali hapa, Kitabu cha Ufunuo, kiliandikwa, mnaona, mwishoni mwa wakati wa kanisa.

122 Sasa, nina jambo fulani dogo hapa ninalotaka kutatua kwa ajili ya jambo fulani ambalo limekuwa ni tatizo la muda mrefu miongoni mwa Wakristo wengi. Nami niliwazia leo, nilipokuwa nikisoma, nikiyaandika Maandiko, na kutafuta majina na rangi mbalimbali na kadhalika. Tutazifikia baada

ya kitambo kidogo, pinde za mvua na mifano, na kadhalika. Nilikuwa nikiyaandika Maandiko haya hapa kusudi niweze kuyaangalia tena na kuyarejea, ikiwa mimi. . .tunapoendelea. Maana, kwa kawaida, kama nilikuwa nikitaka kuzungumzia jambo kama hili, ningeninii. . .ingekuwa ni tofauti, ningejaribu kulijua kimoyomoyo. Lakini kwa njia hii, wakati unapokuwa na wakati mdogo tu, ningetaka kulirejea maana limeenea kote katika Maandiko, huku na huku.

123 Sasa, katika Mathayo 16:13, tunaona hili, kama ninyi ambao mnayaandika Maandiko. Mathayo. . . Ukitaka kurudi. . . ukitaka kuifungua, vema, Mathayo 16:13. Ni. . . Loo, tutageuka tu na kusoma, ndipo tutalipata vizuri kabisa. Mathayo mlango wa 16, na kifungu cha 13. Sikilizeni kwa makini sasa tunaposoma 16:13, "Petro alipokuja. . ." Ama:

> *Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria Filipi, akawauliza wanafunzi wake akasema, Watu hunena. . . Mimi Mwana wa Adamu kuwa ni* nani?
>
> *Wakasema, Wengine hunena. . .u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia,* na, *au mmojawapo wa manabii.*
>
> *Akawaambia, Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?*
>
> *Simoni Petro akajibu akasema, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.*
>
> *Yesu akajibu, akamwambia, Heri wewe, Simoni Baryona: . . .mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni.*
>
> *Nami. . .nakwambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala malango ya kuzimu hayatalishinda.*
>
> *Nami* sasa. . .*Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni: na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni:. . . na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.*
>
> *Ndipo alipowakataza sana wanafunzi wake wasimwambie mtu yeyote ya kwamba yeye ndiye Yesu Kristo.*

124 Sikilizeni kwa makini sasa. Vema. "Kwa kuwa wakati ulianza. . .Tangu wakati huo akaanza. . ." Ninataka mfungue kingine, mnaweza kukisoma chote, fungueni kifungu cha 28 hapa, maana mnaweza kusoma hayo mengine mtakapofika nyumbani.

> *Amin—Amin, nawaambieni, Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa,* mpaka *watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika ufalme wake.*

125 Loo, wazieni hilo! "Wengine wasimamao hapa, *wengine* wasimamao hapa, hawataonja mauti hata watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika Ufalme Wake." Ni tamshi la jinsi gani! Jinsi ambavyo mkosoaji anapenda kulichukua hilo na kuonyesha tu jinsi alivyo mpumbavu, mnaona. Jinsi anavyopenda kulishika hilo, nalo limekwisha kutimia nao hawajui lolote kulihusu. Mnaona? Vema.

126 Baada ya maungamo ya mwamba ya Petro, ambapo tunajua ya kwamba maungamo yake ni . . . Yeye angelijenga Kanisa Lake juu ya mwamba uu huu. Sio Petro, akiwa jiwe dogo, kama vile Katoliki ya Kirumi inavyojaribu kulisema. Bali maungamo ya Petro ya ule Ufunuo, hilo ndilo Kanisa. Mungu atalifunua; sio maungamo ya mtu huyu, kwa sababu baadaye alirudi nyuma. Sio maungamo ya Yeye kuwa ni Mwana wa Mungu; kwa sababu walijua Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, Petro alilisema tu. Bali kitu chenyewe, kilikuwa, ule Ufunuo uliokuwa umefunuliwa kutoka Mbinguni ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Kasema, "Nyama na damu hazijakufundisha hilo, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia. Na juu ya mwamba huu, hayo maungamo mwamba, nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayatalidhuru . . . hayatalishinda."

127 Natumaini hatutaishiwa na wakati upesi sana hapa sasa, tupate kuingilia hili moja kwa moja. Nasi tunataka kuona jinsi hilo linavyotiririka kuingia ndani ya wanadamu. Ni hadithi nzuri papa hapa kama tunaweza tu kuifikia. Vema. Naam, maungamo mwamba, kile Petro alichokuwa . . . Yeye angelijenga Kanisa Lake juu ya maungamo ya Petro. Alisema, "Wengine wasimamao hapa hawataonja mauti hata watakapomwona Mwa—Mwana wa Mungu akija katika Ufalme Wake."

128 Sasa, kumbukeni, Yeye alinena juu ya "wengine." Hao walikuwa ni zaidi ya mmoja, sivyo? *Wengine* wangekuwa ni wengi, "zaidi ya mmoja." Lakini sasa angalieni, wanafunzi Wake wote walikuwa wamesimama pale, Naye alikuwa akimwuliza kila mmoja wao, "Unaonaje juu ya *hili*? Na unaonaje juu ya *lile*?" Bali Yeye alisema, "Pana wengine kati yenu wasimamao hapa, wengine wasimamao hapa, hawataonja mauti kabisa hata watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika Ufalme Wake." Loo, jamani! Ni tamshi la jinsi gani! Wazia, hilo lilitamkwa miaka elfu mbili iliyopita.

129 Itaninii . . . ingeninii . . . Je, Neno la Mungu ni lisiloweza kukosea? Kila Neno asemalo Yeye litatimia?

130 Sasa, tukitaka, tufungue basi mlango wa 17 wa Mathayo ndio unaofuata. Wakati alipochukua . . . Siku chache baada ya hapo, Yeye alimchukua Petro, Yakobo, na Yohana, juu ya mlima, peke yao, wawe shahidi. Petro, Yakobo, na Yohana; nao wakauona Ufalme wa Mungu ukija katika nguvu, walikuona

kule kuja kwa Ufalme wa Mungu kukifanyiwa mazoezi. Amina! Loo, walionyeshwa waziwazi Ufalme wa Mungu ukifanyiwa mazoezi wakati ukija, kule kuingizwa kwa ule Utawala wa Miaka Elfu. Waliona kule kufanyiwa mazoezi.

131 Wakati fulani uliopita . . . kundi la wahudumu, Oral Roberts alikuwa ni mmoja wao. Cecil B. DeMille, hapo alipoandika hii *Amri Kumi,* alimwita Ndugu Shakarian, Ndugu Roberts, wahubiri wengi kote nchini, mhubiri yeyote angaliweza kuja, naye akawaalika kuja kwenye studio kabla hiyo sinema haijaachiliwa, na kuwaruhusu waone masimulizi yake kabla haijaonyeshwa huko nje, wakati walipokuwa wakilipisha dola ishirini na tano kwa tiketi. Lakini yeye . . . Waliona masimulizi yake, wapate kutoa maoni yao kama kulikuwako na ukosoaji wowote kuihusu ama yale yanayoweza kusemwa, na kadhalika. Waliiona kabla umma haujaiona.

132 Naye Yesu alisema, "Pana wengine kati yenu wasimamao hapa" (Amina!) "hawataonja mauti hata watakapouona Ufalme wa Mungu ukija katika nguvu," ama "kumwona Mwana wa Adamu akija katika Ufalme Wake," hasa. "Watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika Ufalme Wake!" Siku chache baadaye, Yeye aliwachukua Petro, Yakobo, na Yohana, wakapanda mlima mrefu, na hapo akabadilishwa mbele zao. Jua, likiwaka, lisingekuwa kama mavazi Yake aliyokuwa amevaa. Ni mara ngapi tumelifafanua katika mifano, tungelifuatilia kote katika Biblia!

133 Unaweza kuchukua fungu moja la Maandiko na kuifunganisha Biblia nzima pamoja kwalo. Naam, bwana. Hakuna kuvuja popote! Yote yamekandikwa kwa nguvu za Mungu. Ibilisi asingeweza kujipenyeza kwake hata akifanya nini. Hiyo ni kweli. Hawezi kuingia kwenye hao watu watakatifu ambao wameweka ushuhuda wao huko nje na kuamini katika Ufalme wa Mungu, na kuchukua kila Andiko na kulikandika kwa nguvu za Roho Mtakatifu, wakaoshwa kwa Damu; ulimwengu hauwezi kuingia ndani yake, ibilisi hawezi kuingia ndani yake. Wamekufa, uhai wao umefichwa katika Kristo kwa Muhuri wa Mungu, kwa Roho Mtakatifu. Ibilisi anawezaje kuwasumbua? Hmm! Hao hapo, katika hali hii sasa.

134 Mahali hapa, basi, yeye aliona kule Kuja, ama mazoezi yake. Basi cha kwanza kilikuwa ni kitu gani, alichoona . . . kitu alichoona? Kitu cha kwanza alichoona katika kule Kuja kilikuwa ni Musa, aliyewawakilisha watakatifu waliokufa ambao wangefufuliwa. Eliya alikuwa amesimama pale.

135 Loo, ninawatakeni muone kitakachotukia. Kulikuwako na Musa, kwanza; hizo ni nyakati hizi zote sita walizolala, nyakati sita za kanisa. Si hilo tu, bali Eliya alikuwako; yule mjumbe wa siku ya mwisho, pamoja na kundi lake, la waliobadilishwa,

Walionyakuliwa. Amina! Sasa katika siku za usoni; wakingojea kule Kuja.

136 Basi wote wanafanya nini. . .? Wote walikuwa wamekusanyika pamoja na Yeye. Loo, jamani! Ilikuwa ni nini? Ahadi yake kwa Petro, Yakobo, na Yohana, ilitimizwa. Hiyo ni kweli. Maana Yeye alisema, "Wengine wanaosimama hapa hawataonja mauti hata watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika Ufalme Wake," nao wakaona mazoezi yake. Ndipo baada ya hili, baada ya kule kufufuka . . .

137 Ningetaka kuwaletea jambo lingine; baada ya Yesu kufa, kuzikwa, katika Yohana Mtakatifu 21:20. Mkosoaji fulani alianzisha jambo hili katika siku za mwanzoni. Papa hapa wakati tukiwa kwenye somo, hebu na tulielezee. Katika Yohana Mtakatifu 20:21, Yesu alikuwa amekutana na wanafunzi Wake, akawalisha samaki na mkate juu ya moto. Nao walipokuwa wakienda ukingoni, Yohana akaegemea kifuani Mwake; naye Petro akauliza swali, kasema, "Itakuwaje kwa mtu huyu?" Yesu alimpenda Yohana, Yohana alikuwa ni mtu wa upendo. Naye akasema, "Itakuwaje kwa mtu huyu? Hali yake itakuwaje? Siku zake za usoni zitakuwaje?"

138 Ndipo Yesu akawaambia, "Imewapasaje kama akikaa hata nitakapokuja, hata nitakaporudi? Ni kitu gani?"

139 Nao wanafunzi wakafanya kosa, wakasema ya kwamba "Yesu alisema kwamba—kwamba—kwamba 'yeye ataishi hata kule Kuja.'"

140 Bali Yesu hakufanya kosa lolote. Papa hapa katika Ufunuo, mlango wa 4, Kristo alilitimiza Neno Lake! Yeye alimleta Yohana hata Mbinguni na kumwonyesha jambo hilo lote. Utukufu! A—aliona onyesho la awali. Yeye aliliona kana kwamba aliishi duniani na kuona nyakati zote za kanisa zikitimia, hata kuja kwa Bwana, Kitabu chote cha Ufunuo. Loo, jamani!

141 Mnaona jinsi ahadi Zake zisivyoweza kukosea? Sasa, wewe umechaguliwa . . . Yakobo kufanya hivyo; Yohana, yeyote wa hao wengine; hata asingemruhusu Paulo kuliona, kulisimulia, hata kidogo.

Alisema, "Inawapasaje kama akikaa hata nitakapokuja?"

142 Na kwa kuwa walisema hivyo, Yeye alimchagua tu Yohana na kumnyakua na kumwonyesha kitu hicho chote kabla hata hajafa, kama tu kwamba aliishi akaona kitu hicho chote. Akamwonyesha jinsi itakavyokuwa! (Ndugu Pat, hilo si ni zuri sana?) Loo, mnaona, akamtwaa moja kwa moja juu. Papa hapa, mlango wa 4 na kifungu cha pili, inaithibitisha. "Alimwonyesha mambo yaliyokuwapo, yaliyopo, na yale yatakayokuja." Alimwonyesha wakati wa kanisa, kuja kwa Wayahudi, kumwagwa kwa yale mapigo, Kunyakuliwa, Kuja mara ya pili, na ule Utawala wa Miaka Elfu, na Makazi

ya Milele ya Waliookolewa Wake; kama tu kwamba aliishi akayaona hayo yote, na kuyaona yote yakitukia. Mnaona? Mnaona? Yeye alimpeleka tu juu na kumwonyesha i—i—ile filamu anayoifungua, akamruhusu kuona kitu hicho chote kikifanyiwa mazoezi. Loo, jamani!

143 Amenyakuliwa. Akaitimiza ahadi Yake katika—katika Ufunuo 4:2. Kabla ya kufa kwake alitwaliwa katika Roho na kuona mambo kama tu kwamba alikuwa ameishi. A—aliyaona yote yakifanyiwa mazoezi. Kwa hiyo aliona, katika ono, kile hasa ambacho kingetukia na kile ambacho kweli kilitukia duniani tangu wakati huo mpaka kule kuja kwa Bwana Yesu. Akamwonyesha katika ono.

144 Kwa hiyo basi hao wanafunzi. . .ama hakuna aliyepata kusema ya kwamba Yeye alisema angekuja katika wakati huo. Alisema, "Imewapasaje kama, (vinginevyo), kama akikaa hata nitakapokuja?" Ndipo akamtwaa juu na kulirudia jambo hilo kwake na kumwonyesha kile kitakachotukia. Loo, ninapenda tu jambo hilo. Hmm. Loo, jamani!

145 Angalieni sasa, hebu tuone hii ilikuwa ni nini:

> *Mara nalikuwa katika roho: na tazama, kiti cha enzi kimewekwa mbinguni na mmoja ameketi* juu yake, juu ya *kile kiti cha enzi.*

146 Kulikuwako na "Sauti" ambayo ilimwita. Loo, Sauti hiyo! Loo, siwezi kuiondokea hiyo, ile Sauti ya Yule nyuma yake. Ndipo akaangalia huku na huku pale, Naye akamwonyesha nyakati zote za kanisa, maana alikuwa amesimama *katika* nyakati za kanisa, vile vinara vya taa saba vya dhahabu. Ndipo akasikia Sauti hiyo baada ya nyakati saba za kanisa kumalizika; hiyo Sauti ikaondoka duniani, ikapaa juu. Alipofika Utukufuni, alimsikia akisema, "Panda hata huku juu! Nitakuonyesha yatakayotukia tangu sasa na kuendelea." Loo, jamani!

147 Sauti hiyo! Hebu tuzungumze juu ya Sauti hiyo kwa dakika moja; ninayo Maandiko yaliyoandikwa hapa. Hebu tufungue Wathesalonike wa Kwanza 4, na tusikilize tu hapa vile Sauti hii itakavyosema. Loo, sote tunajua itakalosema, pasipo. . . kabla hatujasoma, sivyo? Tunajua litakalotukia. "Parapanda ya Mungu italia nao waliokufa katika Kristo watafufuka." Hiyo ni kweli? Ninyi ambao mnaliandika, katika Wathesalonike wa Kwanza 4:16 na 17, "ile Sauti," Sauti hiyo ilikuwa ni Sauti ya Kristo. Hiyo ni kweli? Sauti ya Kristo!

> *Kwa sababu*. . .parapanda *ya Mungu* italia, *nao waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza:*
>
> . . .*sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao*. . . *ili tumlaki Bwana hewani: na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana* milele.

148 Sauti ile ile iliyomwita Yohana, “Panda juu,” Sauti ile ile iliyomwambia Yohana, “Panda juu,” ndiyo Sauti ile ile itakayoliita Kanisa siku moja (Amina!), inayoliita Kanisa.

149 Pia, Sauti ile ile iliyomwita Yohana kupanda juu, ndiyo Sauti ile ile iliyomwita Lazaro aliyekufa kutoka kaburini, Sauti ile ile ya malaika mkuu. Kristo ndiye ile Sauti ya malaika mkuu, “Sauti ya malaika mkuu,” mnaona. Loo, Sauti hiyo ya parapanda ya Kristo ilimwita Yohana apande juu, Sauti hiyo hiyo ilimwita Lazaro. Hivi mliona kwenye kaburi la Lazaro, Yeye alinena kwa Sauti kuu. (Hakusema tu, “Lazaro, njoo huku.”) “*Lazaro, njoo huku*!” Ilimwita kutoka kwa wafu.

150 Naye akajibu, “Mimi hapa.” Naye akatoka katika wafu, baada ya kufa na mwili wake kuoza.

151 Sauti hiyo hiyo ilimwambia Yohana, “Panda hata huku, nitakuonyesha mambo yaliyo karibu kutukia.”

152 Sauti hiyo hiyo itakayolia hapo wafu katika Kristo watakapofufuka, “Kwa maana parapanda. . .” Parapanda! Parapanda ni kitu gani? Sauti ya Kristo, ile ile Ambayo ililia na kumwita apande juu. Yeye alisikia Sauti kama ya baragumu ikilia na kusema, “Panda hata huku!” Mnaona jinsi ufufuo utakavyokuwa? Utakuwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho. Sauti hiyo dhahiri, Naye ataliita Kanisa, akiita, “Tokeni kwake.” Sauti hiyo kuu inayoita. Mungu, nisaidie nikaisikie siku hiyo.

153 Kama vile nimesema mara nyingi. . .Ninajua, kama mwanadamu, Rodney, ninajua ya kwamba kuna mlango mkubwa mweusi uliowekwa mbele yangu, unaitwa mauti. Kila wakati moyo wangu unapodunda, niko mdundo mmoja karibu zaidi na mlango huo. Baadhi ya siku hizi sina budi kuingia ndani yake. Ila sitaki kwenda kama mwoga, nikilia na kupiga mayowe. Ninataka kwenda katika hili, nikijivika mavazi ya haki Yake, nikijua jambo hili: kwamba ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake; ya kwamba siku moja wakati atakapoita, nitatoka miongoni mwa wafu; wakati atakaponiita nikaonekane huko Juu, parapanda ya Mungu itakapolia nao waliokufa katika Kristo watafufuka, kama nitakuwa hai, nitabadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, nami nitaenda pamoja na hao wengine, huko juu kumlaki Bwana hewani. Hiyo Sauti ya parapanda, italia dhahiri, kwa sauti kuu. Huum. Loo, itakuwa ni vile vile katika Kuja Kwake.

154 Hakuna sauti isiyojulikana Kwake. Hakukuwa na kitu kisichojulikana kwa Yohana wakati aliposikia Sauti hiyo ikisema, “Panda huku!” naye akaja. Amina.

155 Wakati Lazaro, katika wafu, kaburini; nayo nafsi yake, safari ya siku nne mahali fulani, sijui mahali ilipokuwa, sidhani yeyote wetu anajua. Popote ilipokuwa, haikuleta tofauti yoyote. Yeye alifanya wito mmoja tu kwa mtu ambaye mabuu ya

ngozi yalikuwa yakiula mwili wake; ananuka, kaburini. Hiyo Parapanda iliyosikika dhahiri ilisema, "Lazaro, njoo huku!" Hapo mtu, aliyekuwa amekufa na kuoza, akajitikisa na kutoka kaburini, akitembea. Hakuna kisicho dhahiri kuhusu hilo, sivyo, ndugu? Hakuna kisicho dhahiri hapo!

156 Ni jambo lile lile usiku wa leo, wakati Sauti inayosikika dhahiri inaposema, "Ewe mwenye dhambi, tubu, nitakupa Uzima wa Milele." Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo miito. Hakuna utata kulihusu Hilo.

157 Mimi ni shahidi kwamba ni kweli. Wapo mashahidi wengine, mamilioni yao kote ulimwenguni leo hii, ambao ni mashahidi kwamba ni Kweli. Wakati Biblia inapokuja, Maneno ya Mungu, kila Neno la Mungu ni parapanda. Kila sauti ya Neno ni parapanda, parapanda ya Injili. Na wakati inapolia, ni Kweli. Wakati iliposema, "Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele," hakuna kisichojulikana kuhusu Hilo. Ni yeye yule! Naam, bwana.

158 "Tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Hakuna kisichojulikana kuhusu Hilo.

159 "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo atakuwa hai. Yeye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Unasadiki haya?" Hakuna utata kuhusu Hilo, "Ataishi!"

160 "Yeye ailaye nyama yangu na kuinywa Damu yangu yuna Uzima wa Milele, Nami nitamfufua tena katika siku ya mwisho." Hakuna kisichojulikana kuhusu Hilo; hakuna; ni sauti ya hakika.

161 Loo, ninaijua, niliisikia ikilia kwenye maskini moyo wangu wa Kiairishi siku moja, mimi, maskini mwenye dhambi. Ingenifanyia namna gani kamwe? Lakini niliamini ilikuwa ni sauti ya hakika, nikaikubali. Mimi ni shahidi kwamba Hiyo ni ya kweli.

162 Siku moja Yeye ataita tena, tutatoka ulimwenguni. Kwa sababu hakuna utata kwa parapanda *hiyo*. Naam, bwana. Naam, bwana, hakuna sauti isiyojulikana, wakati wowote.

163 Yeye hutoa sauti leo hii wakati anapotuita, ni vivyo hivyo anapotwambia lolote.

164 Sasa, hebu turudi kwenye kile kifungu:

> *Na . . . tazama, kiti cha enzi kimewekwa mbinguni . . .* (kifungu cha pili) . . . *na mmoja ameketi juu* yake.

165 Angalieni, "Kiti cha enzi," aliketi kwenye Kiti cha enzi. Hakuwa tena huku chini katika vile vinara vya taa sasa,

duniani. Unyakuo ulikuwa umekuja. Alikuwa Utukufuni, ameketi kwenye Kiti Chake cha Enzi. Ninataka muone huku chini, tutaona hata katika mlango wa 5, hakikuwa ni Kiti cha Enzi cha rehema. Hakikuwa ni Kiti cha Enzi cha rehema tena, kilikuwa ni Kiti cha Enzi cha hukumu. Hakikuwa ni Kiti cha Enzi cha neema, kilikuwa ni Kiti cha Enzi cha hukumu kwa maana moto na umeme na ngurumo zilitoka kwake; hakuna tena, rehema imekwisha, wakati wa Kanisa umekwisha. "Aliye mchafu azidi kuwa mchafu; aliye mwenye haki azidi kuwa mwenye haki; aliye mtakatifu azidi kuwa mtakatifu bado," sio tena Kiti cha Enzi cha rehema.

166 Usiku wa leo, Damu ipo kwenye kile Kiti cha Enzi na ni kiti cha rehema kwa kila mwenye dhambi anayetafuta rehema. Lakini kwenye siku hiyo, hakitakuwa ni kiti cha rehema tena, kitakuwa ni kiti cha hukumu pamoja na Mungu mwenye hasira ameketi pale. "Wapi. . .Kama mwenye haki ataokolewa kwa shida, mwenye dhambi na aliye mwovu wataonekana wapi?" Hata atakapokuja katika mawingu ya utukufu Wake, milima itajaribu kupata mahali pa kujificha. Tutakaa wapi *sisi*, basi?

Loo, mtiririko huo ni wa thamani
Unaonifanya mweupe kama theluji;
Sijui chemchemi nyingine,
Ila Damu yake Yesu.

167 Loo, jamani, ni somo la jinsi gani! Hakuna sauti inayotatanisha! Na Kiti Chake cha Enzi:

> . . .*na* Yeye *ameketi juu ya kiti* Chake. (Hayuko tena hapa.)

168 Sasa, hilo ni jambo lingine, ni thibitisho ya kwamba Kanisa linatwaliwa juu kabla ya ile Dhiki Kuu. Mnaona? Kwa nini? Huyu hapa kwenye Kiti cha Enzi Utukufuni, nalo Kanisa limeondoka, ndipo ile Dhiki inakuja.

169 Sikuzote nimesema ya kwamba katika siku za Nuhu, Nuhu alikuwa ndani ya safina kabla tone moja la mvua kuanguka. Lutu alikuwa nje ya Sodoma kabla moto kushuka. Nalo Kanisa litakuwa Utukufuni kabla ya atomiki kuanguka. Hiyo ni kweli, kabla ya atomiki kuanguka.

170 Unasema, "Na ile ya kwanza je?" Ilikuwa juu ya makafiri, sio Wakristo.

171 Sasa, angalieni. Loo! Yeye amemaliza kazi Yake duniani na amelichukua Kanisa Lake, na sasa anaituma hukumu. Ulimwengu ulimkataa, Naye anatuma hukumu Yake. Yeye pamoja na Kanisa Lake wameenda Utukufuni.

172 Yohana, kule kwenye kisiwa cha Patimo, mfunuzi kwa kanisa, amekuwa ni mfano wa Kanisa ambalo limeinuliwa hata Utukufuni, "Njoo hata huku!" Ikionyesha . . .

Mnasema, "Ati aliliwakilisha Kanisa?"

173 Kwa kila mtu anayelisikia Neno hili, Yohana alimwakilisha. Amina! Yohana alikuwa ni mwakilishi wa Damu ya Yesu Kristo, ule ushuhuda wa Neno. Alikuwa ni shahidi wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, pamoja na ushirika wa kibinafsi pamoja na Kristo, naye aliliwakilisha Kanisa lote; kwamba, kila mwanamume au mwanamke, mvulana ama msichana aliyewahi kumwamini Kristo, akamkubali kwenye misingi ile ile, siku moja ataitwa, "Njoo huku juu!" anyakuliwe kabla ya ile Dhiki. Kumbukeni, ule wakati wa Dhiki haujaanza bado.

174 Huu ukiwa ndio ule wakati, kule kuwekwa kwa ile hukumu. Yohana anaonyeshwa sasa kile kitakachotukia baada ya wakati wa Kanisa. Mnaona? Ndivyo ilivyokuwa.

175 Sasa, angalieni tena katika kifungu cha 3, ama cha pili, "Kiti cha Enzi kilichowekwa Mbinguni, na Mmoja ameketi juu ya Kiti cha Enzi." Sasa, Roho yule yule aliyekuwa duniani, alikuwa ameondoka na kwenda Utukufuni, na alikuwa ameketi (Yesu yeye yule aliye pamoja nasi usiku wa leo) katika rehema, alikuwa ameenda Utukufuni na ameketi juu ya Kiti cha Enzi.

> *Naye aliyeketi* juu ya Kiti cha Enzi *alionekana mithili yake* kama *jiwe la yaspi na . . . akiki: na upinde wa mvua* ulikizunguka *kile kiti cha enzi, ukionekana mithili ya zumaridi.*

176 Nitaondoka, maana kuna ndugu wengine watakaohubiri.

Labda nitalichukua hili asubuhi, papa hapa. Na kwa hiyo, "ukionekana mithili ya zumaridi." Loo, jamani! Loo!

> Wapo watu karibu kila mahali,
> Ambao mioyo yao yote inawaka moto (Hivi hamlipendi hilo?)
> . . . moto ulioshuka kwenye Pentekoste,
> Uliowasafisha na kuwafanya safi;
> Loo, unawaka sasa moyoni mwangu,
> Utukufu kwa Jina Lake!
> Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao.

177 Yonana, aliyeitwa na kuagizwa na Bwana Yesu, aliahidiwa na Mungu huko nyuma kwamba angekuona kuja kwa Mwana wa Adamu. Petro, Yakobo, na Yohana, na hao wengine wakiweko, wakati Yesu aliponena nao na kusema, "Wapo wengine wanaosimama hapa ambao hawataonja mauti hata watakapomwona Mwana wa Adamu akija." Yeye hakusema "wote" waliokuwa wamesimama pale, bali "wengine." Nao wakaenda, siku chache baadaye, na kuona utaratibu wa ufufuo ukifanyiwa mazoezi, na kule kuja kwa Bwana.

178 Eliya aliwakilisha watakatifu waliokufa . . . Ninamaanisha Musa, na kufufuliwa. Eliya aliwakilisha kundi lililohamishwa. Kumbukeni, Musa alikuwa wa kwanza, na kisha Eliya. Eliya alikuwa awe ndiye mjumbe wa siku za mwisho, ili kwa

yeye na kundi lake ungekuja ufufuo. . . ungekuja ninii. . . vema, ungekuja Unyakuo, namaanisha. Musa alileta ufufuo na Eliya akaleta kundi Lililonyakuliwa. Na, hapo, wote wawili waliwakilishwa papo hapo.

179 Ndipo baada ya kitambo kidogo wakatazama basi, nao wakaona, naye Petro akasema, "Na tujenge vibanda vitatu. Acha wengine waende chini ya torati, na wengine waende chini ya Eliya, na hebu twende (baadhi yao) upande *huu*."

180 Basi walipokuwa wangali wakizungumza, Sauti ilinena na kusema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, msikieni Yeye." Nao walipoangalia, walimwona Yesu pekee, kila kitu kilikuwa kimefifia kikawa Kimoja. Loo, Naye alikuwa ni Nuru, Kweli, Njia, Mlango, Upinde wa Mvua.

181 Loo, kesho tuna somo kuu, Bwana akipenda. Kesho tutachukua "hukumu"; tutachukua "jiwe la akiki," tuone kile linachowakilisha, kazi yake. Pia tutachukua li—li—lile la "yaspi" na tutachukua. . . mawe yote mbalimbali, nasi tutachukua haya yote kote kupitia kwa Ezekieli, turudi katika Mwanzo, turejee kwenye Ufunuo, tuje katikati ya Biblia, tuyafunganishe pamoja, mawe haya mbalimbali na rangi, na kadhalika. Kisha tutayarejesha moja kwa moja kwenye hilo tuone iwapo hilo si kweli. Mnaona? Tuone kama si rangi ile ile na kila kitu, kitu kile kile. Naye Roho Mtakatifu yule yule, Mungu yule yule, akionyesha ishara zile zile, maajabu yale yale, akifanya jambo lile lile kama tu alivyoahidi!

182 Yeye aliwaambia Petro, Yakobo, na Yohana, na hao wengine waliosimama pale, wanafunzi Wake wote, kasema, "Wengine wenu hawataona mauti mpaka watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika Ufalme Wake."

183 Kamwambia Yohana, kasema. . . Petro alisema, "Utafanyaje naye? Yeye. . . Jamaa hu—huyo, itakuwaje kwake?"

184 Akasema, "Inawapasaje kama akiniona Mimi nikija?" Naye akamwacha aishi kukuona! Wengine wakiisha kufa na kuondoka, Yohana aliishi kuona kuja kwa Bwana kukifanyiwa mazoezi katika nguvu, mandhari yote imewekwa tangu wakati wake hata kumalizika kwa ile Hukumu na ule Utawala wa Miaka Elfu umeanzishwa. Yohana aliona kila sehemu yake, na ule Utawala wa Miaka Elfu umekwisha, na Wakati wa ule Ufalme ukaanza. Kwa hiyo Yeye hutimiza Neno Lake, sivyo?

185 Tutalitia alama kwenye kifungu cha pili. Bwana akipenda, tutaanzia kwenye kifungu cha 3 asubuhi.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

186 Ni wangapi usiku wa leo, katika kanisa hili, wanaojua, ndugu yangu, ya kwamba, (dada), ya kwamba utaitwa siku moja, uwe tayari ama usiwe? Kama umejiweka tayari ama la, utaitwa kwenda kukutana na Mungu. Parapanda hiyo italia;

na itakapolia, itatoa sauti ya hukumu kwako, mahali ambapo hutaishi tena nawe utateswa katika mashimo ya ibilisi ya kuzimu kwa labda mamilioni ya miaka, ama itakuita huko Juu ukawalaki Watakatifu waliotukuka.

187 Hakika tu kama vile Mungu alivyolitimiza Neno Lake kwa Petro, Yakobo, na Yohana; hakika tu kama vile alivyolitimiza kwa mpendwa Yohana, mfunuzi; hakika tu kama vile alivyoitimiza ahadi Yake kote katika nyakati za kanisa; ni hakika hivyo kwamba aliahidi katika siku hizi za mwisho atatuma mvua ya vuli na atamrudisha Roho yule yule aliyekuwa juu ya nchi ndani Yake, Nuru itakuja wakati wa jioni na kuonyesha Nguvu zile zile, ishara zile zile, na kila kitu alichofanya katika siku Zake angezionyesha tena katika "Mlango huu uliofunguliwa" katika siku za mwisho.

188 Hii hapa! Tunaye moja kwa moja pamoja nasi sasa, Roho Mtakatifu, Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Wewe ni . . . Anawahubiria, anawafundisha, anajaribu kuwafanya muone yaliyo mema na mabaya. Ni Roho Mtakatifu Mwenyewe akinena kupitia midomo ya wanadamu, akifanya kazi miongoni mwa wanadamu, akijaribu kuonyesha rehema na neema.

189 Na wewe hujampokea bado, na kwenye usiku huu wa Mkesha wa Mwaka Mpya ungetaka kuinua mikono yako kwa Mungu na kusema, "Mungu, jalia nipokee Nguvu zilizokuwa juu ya Yohana mfunuzi, kwamba wakati nitakapoitwa nitaonekana mbele Zako katika amani kama alivyofanya?" Inua mkono wako. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Kote kanisani tu. Mungu awabariki. "Jalia niwe tayari kuitikia miito yangu."

190 Baba yetu wa Mbinguni, wakati Mkesha huu wa Mwaka Mpya . . . yapata saa mbili tu sasa na utakwisha, kutakuwa na mwaka mpya. Yale ambayo tumefanya mwaka huu tumefanya. Mambo mengi ambayo nimefanya, ambayo, ninajionea aibu; ninayatubia hayo, Bwana.

191 Pia kuna mambo mengi ambayo nimefanya ambayo wengi wa ndugu zangu hawakuyaelewa. Wengi wa ndugu zangu huko nje hudumani hawaelewi ni kwa nini nimeyafanya. Lakini, Baba, niliyafanya kwa sababu niliongozwa kuyafanya. Ninaomba, Baba, ya kwamba kamwe Wewe hutaniacha niaibike kwa uongozi huo. Lakini endelea kuniongoza, Bwana, kuendelea kufanya kama ninavyoongozwa kufanya. Nisaidie, Mungu, kwa kuwa kwa unyofu ninatafuta kujua mapenzi Yako, kusudi niweze kuyafanya kuwaletea (kama ulivyonionyesha miaka mingi iliyopita nilipoliacha kanisa hili) watu wa ulimwengu Mkate wa Uzima. Wakati nilipouona ule mlima mkubwa wa Mkate, na Watakatifu waliovikwa mavazi meupe wakitoka kote ulimwenguni kula Mkate huu wa Uzima. Ee Mungu, nijalie—Ee

Mungu, nijalie kamwe, kamwe nisikose kuwalisha watu Mkate wa Uzima.

192 Wabariki hawa watu wenye njaa humu ndani walioinua mikono yao sasa hivi. Wanatafuta Uzima zaidi. Ninaomba kwamba utawajaza na Roho mtakatifu, Bwana, kila mmoja wao. Mungu, tujalie. Wape baraka. Wasaidie ndugu zetu, kila mahali.

193 Wabariki ndugu zetu wahudumu wanaojiandaa kuja huku tena, sasa katika dakika chache, wengine watakuwa wakizungumza. Tunaomba ya kwamba watatupatia Mkate wa Uzima usiku wa leo, Baba, wakati tukisikiliza kwa makini na kwa uchaji kuisikia ile Sauti. Tujalie.

194 Tubariki. Na ujalie mwaka huu mpya upambazuke kwa matumaini mapya, ukileta mawazo mapya, funuo mpya, nguvu mpya, loo, kila kitu. Jalia zifanywe upya kwetu tena, Bwana, baraka na ahadi Zako. Tunajikabidhi, kwa maombi yetu, mikononi Mwako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Asanteni, ndugu zangu na dada.

195 [Ndugu Neville anazungumza: "Nina hakika sote tunaweza kushangilia hatukuwa na haraka hata kidogo na tungefurahia sana kuendelea tu kusikiliza; kumsikiliza Ndugu Branham hapa usiku wa leo akituletea ujumbe huu. Na ni ujumbe unaotutia moyo kwa kuwa tunajua Mungu yuko ndani yake. Amina."—Mh.] Bwana asifiwe! ["Na yale Yeye amesema anaweza kabisa kuyatimiza hata kuja Kwake tena."] Naam. ["Naye atayatimiza, si hivyo tu, mara nyingi nimesema ya kwamba . . . mara nyingi tunawaambia watu, 'Je, unaamini ya kwamba Yesu Kristo anaweza kukuponya?' na, hakika, kwa kawaida unaweza kuwafanya walikubali hilo. Lakini jambo ni kwamba, je, unaamini Yeye atakuponya sasa?"] Amina! ["Ndipo wakati mwingine watu husema, 'Vema, sijui mimi.' Yule mama ambaye ndio kwanza aage dunia hospitalini; nilienda kumwona, kasema, 'Dada, ungali unaamini ya kwamba Yesu huokoa?' Akasema, 'Naam, ninaamini.' Nikasema, 'Unaamini ya kwamba Yesu Kristo huponya?' Akasema, 'Naam, bwana, ninaamini.' Nikasema, 'Unaamini Yeye anakuponya sasa hivi?' Akasema, 'Hilo sijui.' Nami nikasema, 'Dada, unaweza kujua kwa sababu hiyo ahadi ni kwa ajili yako.'"] Amina! ["Amina. Yeye ametoa hiyo ahadi. Sasa, wakati tukienda kumsikiliza mwingine wa ndugu zetu hapa. Tunao kadhaa mahali hapa na huu . . . Kwenye Mkesha huu wa Mwaka Mpya, hatuna ratiba iliyopangwa awali. Tunakusanyika tu pamoja na kumwacha Mungu atende kazi anapotuelekeza na kutuongoza."] Amina! ["Nanyi mwajua, imekuwa ni muda mrefu sana tangu tulipomsikiliza Ndugu Pat Tyler na kutoa ushuhuda wake wa chochote Bwana atakachoweka moyoni mwake. Nasi tutamwomba Ndugu Pat alete chochote Mungu anachoweka moyoni mwake. Lakini kabla hajaja huku, ndugu mzuri Mkristo huko nyuma, Ndugu Randall

Hyman, naye yuko hapa na ana talanta ya Bwana kuimba nanyi mwajua. Nimetamani tu aweze kuitumia talanta hiyo kwa Utukufu wa Mungu, kwa hiyo nitamwomba Ndugu Randall kama angeweza kuja huku juu na kutuimbia. Ametuimbia mara moja ama mbili hapa nami nitamwomba aitumie talanta yake tena usiku wa leo kwa ajili ya Bwana Yesu, akipenda. Kama atakuja sasa kutuimbia. Ana watoto huko nyuma anaosaidia kuwashughulikia, lakini labda anaweza kuwaondokea sasa na kuja huku na kutuimbia. Wakati akifanya hivyo, pia tunaye Ndugu Kinder hapa nyuma; ndugu mpendwa wa Kipentekoste, tunamfurahia. Pia tunaye Ndugu J. T. Parnell huko nyuma mahali fulani. Nafikiri ameketi papa hapa nyuma nje ya safu. Nasi tuna furaha sana kwa ajili ya ndugu hawa wote Wakristo wema . . . "] Beeler pale. [" . . . ndugu wa imani na hebu tuone."] Ndugu Beeeler yuko kule nyuma. ["Ndugu Beeler yuko hapa nyuma, pia. Naam. Ndugu Beeler yuko hapa na . . . "]

Ufunuo, Mlango Wa Nne Sehemu Ya I SWA60-1231
(Revelation, Chapter Four Part I)
Mfululizo wa Ufunuo Wa Yesu Kristo

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumamosi jioni, tarehe 31 Desemba, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org